

CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

(CKRC)

VERBATIM REPORT OF

CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS,

SIGOR CONSTITUENCY,

AT KIBICHBICH D.O.'S OFFICE

ON

Monday 1st July 2002

CONSTITUENCY PUBLIC HEARING SIGOR CONSTITUENCY

MONDAY 1ST JULY 2002 AT KIBICHBICH D.O.'S OFFICE

Present:

Com. Ibrahmi Lethome

Com. Bishop Kariuki B.N. Karuiki

Secretariat:

G. Nakholi - Programme Officer

Wambua Kigame - Assistant Programme Officer

M. Babu - Verbatim Recorder

William - 3cs Member

Pius Lokita

The meeting was called to order at 9.55 a.m, with Commissioner Lithome in the chair.

William: Tunataka tuanze mara moja. Sijui watu wamekuwa tayari. Muko tayari? Basi commissions wetu, Bishop Njoroge, na

team yake ambao mumefika asubuhi ya leo, mimi kwanza kitu ya kwanza nitafanya ni ku-introduce wale C.C.C. members, ingawa mmoja ameenda kuangalia public address system. Kwa hivyo, kabla sijafanya introduction ya C.C.C. members, naomba mtu mmoja, Pastor mmoja atuongoze kwa maombi. Pastor.

Samuel Achogole: Mimi ni Mwinjilisti Samuel Achogole katika kanisa la A.C.K. hapa Lalale. Tuombe. Baba mfalme, Mungu uiishie milele tunakushukuru Mungu asubuhi ya leo kwa maana imekuwa ni siku njema, tukikumbuka katika historia ya nchi yetu ya Kenya tangu tupate uhuru, hata kuumbwa kwa ulimwengu, kuweza kupata nafasi ya kuwa pamoja na ma-commissioners ambao wanahusika, na kuandika katika Katiba yetu ya Kenya. Tunakuomba baba, tunasema asante Mungu wetu kwa kutufikiria, ili tuweze kuwa miongoni mwa wa Kenya wengine kutoa maoni yetu. Tunakuomba Mungu uwe pamoja nasi katika kikao hiki, na uongoze kila mwananchi. Uongoze kila mtu ambaye atakuja kusema yale ambaye anaona kwamba yanafa ili yaweze kutolewa, na kiweze kuwa chombo cha maana katika Katiba yetu ya Kenya. Asante Mungu kwa kuongoza ma-Commissioners wetu, ambao wametoka Nairobi kupitia katika anga, kwa chombo ambacho kiliundwa na binadamu, kwa kuwafikisha mahali hapa ili tuweze kushirikiana pamoja. Tunakuomba baba roho wako mtakatifu, aweze kuwa nasi katika kikao hiki, ili utuongoze mpaka mwisho tukikushukuru katika yote, kwa jina la Yesu Kristo, mwokozi wetu. Amen

Audience: Amen

William: Basi nafikiri wale members wa C.C.C. walioko hapa, kuja karibu. Huyu aliyekaribu hapa ni Mary Selongole, ni mmoja yao wa C.C.C. member, ya Sigor Constituency na mmoja ambaye anaitwa Goeffrey Lokudo ameenda kuangalia public system mahali, na atakuja. Sisi watatu peke yake ndio tuko upande wa Lela, na wale wengine wanapatikana upande wa Sigor. Kwa hivyo area hii ni kubwa kabisa, mpaka Sigor ni mbali tukagawa kazi., tukasema sisi tuwe katika Highlands, na wale wawe katika Lowlands. Kwa hivyo karibuni sana.

Basi kabla hatujaendelea ningependa kukaribisha diwani kama kiongozi au Senior Chief atoe neno. Councillor kuja, zungumza, karibisha watu hapa, ili mimi niendeleo na sehemu zingine. Au unaona aje? Karibu, karibisha na neno mbili basi tuanze kazi.

Cllr.: Asante sana. Kwanza commissioners wetu wa marekebisho ya Katiba, wananchi, commissioners tunasema karibuni, karibuni kabisa. Tunafurahi, sisi pia tunataka kusema asante, kwa sababu mmekuja mpaka ndani yetu. Kwa hivyo sisi tunafurahi na kusema asanteni karibuni, sikiza maoni yetu kabisa, mpaka ya mama, mpaka ya nani, kila mtu. Kwa hivyo tutatoa yale tunaweza, kwa hivyo tutajaribu wakati ili tumalize pamoja, na mimi nafikiri saa hii watu bado wanakuja. Msikuwe na haraka sana kufikiria tumechelewa. Nchi ya baridi kawaida, watu huchelewa kidogo, lakini hio sio hoja watakuja tu. Kwa hivyo asanteni sana.

William: Basi ma-commissioners na wale wageni wote ambaye wamefika hapa nikuaza sasa Kabla sijakaa chini, napenda kusema kwamba tunashukuru Mungu kwa sababu maombi yetu yamesikizwa na commissioners wetu, hakuna moja

amekanyanga hapa wakati ingine tangu azaliwe. Lakini Mungu amewaleta mpaka leo hapa, kwa hivyo karibuni sana.

Kitu ambacho nitafanya sasa, ni kumpa jukumu mwenyeki ambaye ni commissioner mmoja aongeze taratibu ya leo. Lakini kabla commissioner sijampa yeye, Bwana Pius Lokila ndiyo mkalimani wetu, yeye ni interpreter, kwa sababu hata ukipenda kuzungumza kwa lugha yako, huwezi kuzuiwa. Kiswahili huwezi kuzuiwa, hata Kingereza. Kwa hivyo usiwe na shaka kwamba sijui lugha hii nitazungumza nini. Bwana Pius Lokita atatafsiri yaani ata-translate kwa lugha ya Kiswahili ili ieleweke. Kwa hivyo Bwana commissioner nasema karibu. Sasa nakupa wewe jukumu uendeshe mkutano. Asante.

Com. Lethome: Asante sana Bwana William, hapa mahali mnaitaje?

William: Hapa ni Lela.

Com. Lethome: Lela

William: Kabichbich

Com. Lethome: Sasa watu wa Kabich bich (ki-Pokot) (clapping) Asanteni. Hiyo peke yake ndio nimejifundisha halali (laughter). Kwanza tunamshukuru Mungu kwa kutufikisha salama, na pia kutufikishia siku ya leo. Kama alivyosema William, hii ni siku muhimu sana katika historia ya nchi yetu. Ndiyo mara ya kwanza wananchi wa Kenya wameambiwa, mna uhuru wa kusema mnataka sheria ambaye itakayo watawala iwe namna gani? Na, watu wa hapa mmebarikiwa na Mungu katika sehemu nyingi hi imechaguliwa ni moja katika ile sehemu ambapo commissioners watakuja kuweza kuwasikiza.

Leo si siku yetu ya kuzungumza, leo ni siku yetu ya kuwasikiza nyinyi, na ningependa kuwajulisha wale ambao tumekuja nao hapa. Upande wangu wa kushoto ni Commissioner Bishop Bernard Njoroge, ambaye pia ndio kiongozi wa ile kundi yote ambayo iko upande huu, North Rift, yeye ndiye anaongoza. Ningependa awaamkue.

Com. Bishop Kariuki Njoroge: Hamjambao wananchi?

Audience: Clapping

Com. Lethome: Haya asanteni, lakini usije na helicoper ya kubomoa skuli, inabomoa skuli. Halafu tuna officers kutoka katika ofisi yetu kuu ambao wanashirikiana na sisi. Upande wa mwisho kabisa kuna George Makholi, yeye ni Programme Officer. Ndio msimamizi wa idara, administration yetu yote yeye ndiye anaisimamia. Baada ya mtu kutoa maoni yake, Bwana Makholi ana-register moja ambayo ni ya historia kabisa. Itakaa hata mpaka wale watoto hawajazaliwa, wakizaliwa watakuwa wanaona kwa Sigor mahali Fulani, hawa ndio waliozungumza na hizi ndio signature zao. Kwa hivyo ukishazungumza utakwenda pale

Bwana Makholi atakuonyesha mahali utaandika jina lako, address yako, na utaweka kidole yako. That is a historical record. Miaka na miaka, madamu Kenya inaendelea, your name will remain in that record. Ndio nawambia hii ni historia. You are making history today in this place. Kwa hivyo Mungu ametubariki kuwa sisi na nyinyi tuko hai kutengeneza hiyo historia (clapping)

Halafu tunae Bwana Wambua (clapping). Huyu kijana aliye hapa katikati anaitwa Wambua. Kazi yake ni ku-record kila kitu ambacho mnazungumza, ana-record kwa maadishi. Wambua wamkue watu wa Sigor.

Wambua Igame: Hamjambo nyote?

Audience: Clapping

Com. Lethome: Halafu mwisho kabisa kuna Mary, Mary kazi yake ni mashini. Ako na hizi mashini mbili. Hizi mashini hata ukikohoa huko nyuma inashika maneno yote. Hata vile huyu mama anatembea saa hizi ina-recordi hapa. Hatutaki neno lolote ambalo mnazungumza lipotee. Kila kitu, hata yale maombi Pastor ametoa yote ita-recordiwa., inapelekwa kwenya library yetu na hayo maneno yatatolewa, yatawekwa kwenye computer. Itakua ni maneno ambayo yataingia katika record yetu, na pia report ile ambayo tutatengeneza ya Katiba. Kwa hivyo Mary ndio kazi yake, Mary wamkue wasiseme nimeonea wa akina mama.

Mary Babu: Hamjambo wananchi?

Audience: Clapping.

Com. Lithome: Kwa hivyo hao ndio tumeshirikiana nao leo. Kama nilivyowaambia leo ni siku yetu ya kusikiza, na si siku yenu ya kuzungumza. Kama alivyosema William, zungumza kwa lugha ambayo unapenda wewe mwenyewe. Zungumza Kiswahili, zungumza Kingereza au Ki-Pokot, nimesikia tukona mkalimani, ili uweze kujieleza vizuri. Usiwache maneno yoyote ambayo unaona ni muhimu sisi tusikie kwa sababu ya lugha. Kwa hivyo tumia lugha ambayo unataka.

Ya pili hakuna kitu ambayo haina sheria. Kwa hivyo hata sisi kikao chetu hapa kiko na sheria. Hata mpira uwanjani uko na sheira. Ama haina sheria?

Audience: Iko

Com. Lethome: Iko na sheria. Sheria yetu ya kwanza; Kuheshimu maoni ya wengine. Hata mama na mzee nyumbani wakati mwingine hawana maoni moja, lakini hawavunji nyumba, hawapigani wanasikizana. Kila mmoja anaheshimu maoni ya mwingine

kwa hivyo akija hapa mtu, kama ni William nimwite hapa atoe maoni yake, hata kama haikukupendeza, hiyo ni maoni ya William. Tumwachie amalize. Akisha maliza, nawewe uje hapa utoe maoni yako. Hio tumekubaliana?

Audience: Ndio.

Com. Lithome: Kwa hivyo nikisikia kelele huko ati kuwa William amesema kitu fulani ambacho sisi hatutaki mimi nitatoa red card kama referee. Nikwambie hio sasa umekwenda off side. Kwa hivyo tumekubaliana tuheshimu maoni ya wengine. Sawa hio?

Audience: Mum

Com. Lethome: Haya, kuna namna mbili ya kutoa maoni. Mimi najua kuwa kuna watu ambao wako na memorandum. Kama huyu mzee mwenye tai nyekundu ako na yake tayari. Ukiwa na memorandum na unataka kuzungumza utakuja hapa kwenye hiki kiti, utasema jina lako, halafu hio memorandum huwezi kusoma yote. Hio ni yetu, ni mali yetu, utatuachia sisi tusome. Utafanya ile kitu inaitwa na Kingereza, highlight. Yale maneno muhimu, utatueleza. Nitakupatia dakika tano ku-highlight hio memorandum yako. Kama hutaki kuzungumza, toa jina lako, sema uko na memorandum, pengine unawakilisha kikundi fulani, halafu unamkabithi Bwana Makholi uta-register huko kwake.

Namna ya pili ya kutoa maoni, ni watu ambao hawana memorandum, kama huyu mama naona hana memorandum, lakini yake iko hapa. Maoni yake yote ya Katiba iko hapa. Atakuja hapa, atasema jina lake, aanze kutoa pointi yake. Na tunasema nitakupatia dakika kumi, na hizo dakika kumi haiwezi kutosha ukianza kutoa hadithi nyingi. Kama unataka kuzungumzia habari ya matatizo ya umeme na muko na Turkwel hapa karibu, sianze kusema sijui Turkwel ilijengwa hapa mwaka Fulani, imetuharibia mambo Fulani, na hatuna umeme. Sema tunataka serikali itupe facilities, hio ni pendekezo moja. Tunataka kitu Fulani. Hiyo tumekubaliana?

Audience: Ndio.

Com. Lethome: Sawa. Halafu nitakupatia dakika kumi ikiwa hauna memorandum. Kisha mimi najua kwa sababu ya historia yetu ya Kenya ambayo tunataka kubadilisha sasa, maneno yote ambayo inahusiana na sheria au serikali, mtu akianza kuzungumza hapa anaangalia chief yuko hapa ama hayuko? D.O. yuko hapa? Kuna askari hapa, kuna special branch hapa? Unaongopa kuzungumza, juu ukizungumza utafuatwa huko. Si ndio hio huwa iko?

Audience: Ndio.

Com. Lithome: Sasa tunawambia hivi, sheria ambayo imeunda hii tume (commission), imetoa uhuru kwa kila Mkenya kusema kile anachotaka, na ukifwatwa kwa sababu ya kutoa maoni yako hapa, sheria imesema huyo mwenye kukufuata anashtakiwa.

Sisi wenyewe tutachukua jukumu ya kumshtaki, kwa sababu sheria imepitishwa na wambunge, imewekwa sahihi na Rais, watu watoe maoni yao vile wanavyotaka bila kuogopa mtu yeyote.

Halafu ma-chiefs wapewe cheo. Halafu ma-chiefs wapewe nguvu na magari na nini isaidie watu. Kama ni wagonjwa nini kwa sababu hawa ndio kiungu kikubwa sana cha kuunganisha wananchi na serikali, lazima wapewe vifaa vya kutosha.

Halafu upande wa security: Katika district security committee, kama ni DC wa Pokot wachague Pokot mmoja awe chairman wa district security committee, kwa sababu hawa ndio wanaelewa sana mambo ya amani na nini, kuliko kuchukua DC ambaye hajui historia yetu, mila yetu, awe chairman. Anastukia tu kama, hii district wanastukia kwamba co-operation inafaa. Sisi tunagongwa kila mara kwa sababu hawajui historia yetu na mila yetu. Kwa hivyo ningependa chairman wa district committee awe ni mwenyeji wa kila upande.

Basi ningependa pia social welfare fund, maslahi ya wazee iangaliwe. Yaani tuwe na senior citizens allowance ya kuangalia wale wazee wamekua zaidi wazee, wapatiwe mshahara. Mwenye ana miaka sabini kuelekea ju, ili wasikufe haraka kwa sababu ya umaskini kwa sababu saa hiyo mtu akishaafikisha miaka sabini anayanganywa shamba, ngombe. Serikali iangalie iwapatie mshahara kidogo kidogo ya ku-sustain hawa.

Com. Lethome: Nani anawanyang'anya shamba?

Johnson Lokita: Watoto wao, hawana nguvu sasa.

Com. Lethome: Basi ungependa sheria iwalinde.

Johnson Lokata: Iwalinde hawa wazee na iwapatie mshahara karibu elfu tano kila mwezi, ili hata Mungu naye afurahi abariki nchi hii.

Basi jambo lingine ni mambo ya chokora. Sheria nayo iangalie mambo ya chokora. Tunaangalia watoto wengi wametapakaa sijui ni umaskini, sijui ni nini, ijengwe maboma halafu ichunge hawa watoto. Wasanywe huko ndani, halafu wasomeshe. Nafikiri ni umaskini ndio unafukuza hawa kutoka nyumbani.

Basi jambo lingine ningependa mambo ya IDS na passport. Passport na ID ipatiwe raia wote. Wale raia wa Kenya, kuliko kusumbua hawa ati tujaze ma-forms, kwa sababu ni wananchi wanajulikana. Wapewe kila mtu passport, akitaka kwenda wapi anaenda bila masharti mengi.

Basi mambo ya land ownership: Ngingependa nchi, yaani kila wilaya, ama kila sehemu, wazee wapewe mamlaka ya kusimamia

ardhi. Kama ni forest wajue wanalinda namna gani, kama ni nini, hata district chairman land board awe ni mwenyeji, isiwe ni DC. Kwa sababu hio sasa mtu akishakua DC watu wengine wanaogopa na hata haki yao wananyanganywa. Ikiwa ni wenyeji sasa ndio wanamamlaka hata wataangalia masilahi ya kila mtu.

Jambo lingine ni individual land ownership: Ningeonelea katika hii constitution sasa hii sheria kila mtu amiliki shamba mpaka mita mia moja chini ya ardhi, isiwe futi mbili vile wanasema. Kwa sababu kama minerals kama iko chini, wasiwanyanganye ile huyo mtu afaidike, na kuwe na land ceiling. Mtu asiwe na acre elfu kumi, na wengine wanaumia kuwa chokora. Kwa hivyo ningeonelea acre mia tano tu ndio iwe ya juu. Yale mashamba mengine yanabaki. Wazee wa kila sehemu waangalie hio shamba, ilindwe kwa minajili ya siku zingine.

Halafu jambo la mwisho, ningeonelea hii tume kama mtakuwa na uwezo, nasi hapa sisi wa-Pokot hapa tupewe 2 constituencies kwa sababu tumekuwa na shida nyingi sana. Constituency kama Lelan Constituency, na Lale ili masilahi yetu yaangaliwe vizuri. Halafu ya mwisho bwana commissioner ni kwamba mambo ya kortini.

Tuwe na korti kama hii ya Katiba, Constitutional Court, Supreme Court of Kenya, Court of Appeal, High Court, Land Claim Court, like in South Africa. Customary Court iwekwe naye manani ili ile wazee wakitaka kitu ijulikane naye hii sheria iko ndani, na hio iangalie customary court (1), iangalie masilahi ya kila mtu, kama land, kama ni communal matters. Halafu customer court (2), iangalie mambo ya familia kama mtu amefanya kosa kwa mahali kama wengine wameweka mimba mtoto, sisi kwa Pokot kuna kitu inaitwa “chula” hiyo iwekwe nayo iwe sheria, kama mtu akiua mwingine katika Pokot tuna kitu kingine inaitwa “lapi” ambaye ni fine, iyo nayo iwekwe manani. Kama divorce mtu akikosana na mkewe, isipelekwe kortini, ipelekwe kortini ya mila, kwa sababu hawa ndio wanajua. Sababu wakipeleka hii ingine basi ujuaji mwingi utatokea na watu wengi watakosana kwa boma. Hio tu ndiyo ningeonelea. President achaguliwe moja kwa moja na asiwe mbunge, na ni kwa maoni yangu ningeonelea lazima awe amewahi kwa governor kwa jimbo moja.

Com. Lethome: (not clear)

Johnson Lokita: Asante kwa hivyo ninamalizia hapo, asante. Ni hayo tu.

Com. Lethome: Asante sana Johnson. Sorry nilipokuwa na introduce watu wote nilisahau mtu mmoja. anaitwa Commissioner Ibrahim Lethome, nilikuwa nimemsahau, nimemkubuka sasa. Nguriareng Kapemilee, karibu mzee. I hope mumetuma mtu wa kuonyesha mahali uta-land usivunje nyumba ingine. Umetuma mtu? Okay.

Nguriareng: Oyokchiinan chichi lee Commissioner soro ompo wolo kemuuk ta kunguun aswaneete koreencha kunguun kuterweecha ngale chaaa. Kurenanun nguriareng Kapelile

Translator Pius Lokita: Anarudisha shukrani.

Nguriareng: Oyokchiinan soro

Translator Pius Lokita: kwa commissioner,

Nguriareng: Commissiner

Translator Pius Lokita: ambaye amekuja upande huu leo,

Nguriareng: Nyo kengun

Translator Pius Lokita: kusikia maoni yetu.

Com. Lithome: (Not clear) Jina lake, jina.

Nguriareng: Nguriareng

Translator Pius Lokita: Anaitwa Nguriareng.

Com. Lethome: Haya endelea tu.

Nguriareng: Tangaa tagh weena

Translator Pius Lokita: Kusikia maoni yetu,

Nguriareng: Kterwecha ngale chaa

Translator Pius Lokita: Kwa sababu tangu hapo awali hakuna aliyesikia maoni ya Wapokot.

Nguriareng: Ompowolo momiteeni nyee chii nyo kikunguun kuterweecha ngale chaa

Translator Pius Lokita: Kwa sababu Mpokot akizungumza hapa awali wanaanza kumluka yeye

Nguriareng: Ompo wolo Pochon mimiitani nyee chii nyo moroy

Translator Pius Lokita: Sasa,

Nguriareng: Klee nyoona

Translator Pius Lokita: Tunasema sasa maoni yetu, ya nchi yetu.

Nguriareng: Kmwaghecha yee nyuu mochuut ko chaa ompo koree ncha

Translator Pius Lokita: Ya kwanza,

Nguriareng: Nyop tagh

Translator Pius Lokita: Ni kuhusu police

Nguriareng: Kuu le nyee ngal police

Translator Pius Lokita: Police wakati unaenda kwa headquarters ya police kama Kapenguria,

Nguriareng: Otoi iwenyii kaa Police lenyee Kapenguria

Translator Pius Lokita: unariporti mali yako ambayo imeibiwa,

Nguriareng: Ato imwotutooneyii kyaakikukuu choo kikichoor

Translator Pius Lokita: sasa unaabiwa utoe pesa.

Nguriareng: Nyo kmowoghwekwaa loo okonuno ropyeen

Translator Pius Lokita: Ya pili,

Nguriareng: nyopo odeny

Translator Pius Lokita: ukienda kwa hospitali,

Nguriareng: Ompo lenye ospitaliin

Translator Pius Lokita: Wewe ni mgonjwa ile ya mahututi,

Nguriareng: Ichiinyi chiirate nyopo toongonjiin

Translator Pius Lokita: sasa wanakuitisha pesa.

Nguriareng: Kelenjiinyi kono ropyeen

Translator Pius Lokita: Sasa utapata wapi pesa ukiwa mgonjwa?

Com. Lethome: Kuhusu mambo ya hospitali?

Nguriareng: Kleenye ngala hospitalii,

Translator Pius Lokita: Mwoghenyii lonee yee nyuu nyaa?

Nguriareng: Omokan ketoo piich sakuut

Translator Pius Lokita: Sasa anaonelea hospitali watu wapate matibabu ya bure.

Nguriareng: Mchiini ketoo piich sakuut

Translator Pius Lokita: Ya tatu,

Nguriareng: Nyopo somok,

Translator Pius Lokita: kuna forest yetu ambayo iko karibu na sisi hapa,

Nguriareng: Miiteni ngala wuudun (foresti) nyo miiteni yii yee

Translator Pius Lokita: kwa maoni yetu tunataka ni sisi wenyewe ndio tunalinda forest yetu hii.

Nguriareng: Kmokeecha kluuku pooy chanee chiini ripoy

Translator Pius Lokita: Ya nne,

Nguriareng: Nyopo angwaan,

Translator Pius Lokita: Tunataka raslimali zetu zote ambazo zitapatikana hapa ziwe zetu, na ziwe mali yetu.

Nguriareng: Kmorecha tukuu chaa kupkaa koreenchaa poo Pokot

Translator Pius Lokita: Ya tano,

Nguriareng: Nyopo Muut

Translator Pius Lokita: Kuna ambao hawajiwezi hata kuweza kusomesha mtoto,

Nguriareng: Miiteni piich cho momuuktonyee kusomeshon monuung,

Translator Pius Lokita: Tunataka pia shule iwe ya bure.

Nguriareng: Kmookecha kungaraak piipo sooch

Translator Pius Lokita: Ni hayo.

Com. Lethome: Asante sana mzee, asante sana. Sasa tumpatie Loshalima Samuel, Samuel, hauko? Karibu.

Loshalima Samuel: Soro nyo wou, karibu wena Losialima

Translator Pius Lokita: Anarundisha shukrani.

Loshalima Samuel: Soro nyo wou

Translator Pius Lokita: Ana maoni mawili.

Loshalima Samuel: Otungoon kinonuut

Translator Pius Lokita: Kuna maji ya chemichemi

Loshalima Samuel: Otungoon ngaal odeny ompuun

Translator Pius Lokita: Tunataka sasa kama mito yetu ambayotuko nayo hapa karibu ambao ina maji mengi, tunataka watu wa power watupatie uwezo ya kumiliki hizo maji, ili sisi tukitafuta hata donor wetu ambae anaweza kutusaidia ijengewe iwekwe hapo electricity power, ili iwe mali yetu.

Loshalima Samuel: Miiteni pogh chopo (chemichemi), kmoorechaa lenye lalwatiin neecha choo miiteni pogh choo chang ompo piipo Kenya Power kukoneecha owesyo nyo kimuukecha keyaar chii nyo ngorokeecha keteek kopo maa (Electricity) kluuku malii-cha.

Translator Pius Lokita: Ya pili,

Loshalima Samuel: Nyopo odeny

Translator Pius Lokita: Tunaona maoni yetu kuhusu county council ni ya kwamba ni watu ambao wanadhai ardhi juu. Kwa maoni yake ni ya kwamba county council wadai ma-plot ya ma-centre tu.

Loshalima Samuel: Kak suweecha loo County Council kuup piich paat cho michiinoy kteep kilipanat nyopo plotiin chopo Centre kulee

Translator Pius Lokita: Wasiwe watu wa kumiliki ardhi yote.

Loshalima Samuel: Mekuutang orii pareen

Translator Pius Lokita: Wadai tu ile manyumba ya biashara.

Loshalima Samuel: Ku waak tukuu biashareen ompun

Translator Pius Lokita: Hio tu ndio maoni yake sasa.

Com. Lethome: Asante sana Mzee Loshalima, kajiandikishe mzee huko. Tumpate sasa Stephen Ynalereng, C.J.P.C.

Stephen Ynalereng: Ya kwanza namushukuru Mungu kwa kuweza kutukutanisha kwa siku ya leo. Ya pili nitawashukuru Ma-commissioners ambao mmeweza kufika. Nasema shukrani kwa sababu tunaona ni history tumeweza ku-record tangu ulimwengu uumbwe mpaka wakati huu. Ni vile mmesikia mimi ni Stephen Ynalereng, nina maneno manne, na nitaharakisha vile

naweza.

Ya kwanza, kuna mtu aliguzia mambo ya forest. Kulingana na mimi, mambo ya forest, iwe inadhamini wa local county council ikiwa chini ya ulinzi ya wazee wa community yetu. 75% ya rasimali yake iende kwa county council yetu. Halafu 25% ikuje kwa county council.

Ya pili, ninaonelea kwamba mambo ya councillors, malipo ya councillors imetufanya sisi na councillors wetu hatuhusiani vizuri, kwa sababu hawalipwi vizuri. Tunawachagua kama councillors, na baada ya kuchaguliwa wanakuwa chini ya wabunge kwa sababu hawana chochote. Kwa hivyo ningeonelea kwamba councillors walipwe jinsi wanavyolipwa wabunge. Ili hao wenyewe wajitegemee na watuhudumie, badala ya kuwa chini ya wabunge na watusahau.

Juu ya uwezo ya President: Naonelea kwamba President awe chini ya sheria, badala ya kuwa juu ya sheria ili tuhudumiwe. Ikiwa mtu anaogopa sheria ya kwamba akienda kinyume ataadhibiwa, badala ya mtu kuona hakuna hukumu juu yake, kwa sababu ako juu ya sheria. Kwa hivyo President awe chini ya sheria kulingana na maoni yangu.

Na ya mwisho ni kuhusu mambo ya provincial administration. Ninaonelea kwamba kuanzia DO mpaka PC hio post hatuoni faida yao. Tunaona ifutiliwe mbali, na badala ya chiefs wapewe uwezo ili waweze kuhudumia wananchi kulingana na vile wanaelewa, kwa sababu ni wenyeji. Ni hayo tu.

Com. Lethome: Asante sana Stephen Ynalereng. Sasa tutabadilisha kidogo mtindo, nataka tupate mama - Mary Chelengole?

Mary Chelengole: Asante sana kwa fursa hii kwa kuleta forum ambayo ni free and fair utoe maoni yako kama mwananchi wa constituency ya Sigor. kwa sababu mimi nawakilisha kina mama siwezi nikasema yale yote ambayo watasema. Ninasema tu maoni yangu, nilivyoandika na nitasoma kwa Kingereza.

Ya kwanza ni preamble: The new Kenyan Constitution should have a preamble that expresses the basic national value, philosophy and the vision to which Kenyan people collectively aspire. In the current constitution we don't have a preamble.

Two, directive principles of state policies: We need statements in our constitution capturing the national philosophy and guiding principles of the state. The following directive principles should be enforced by the law. One: The rule of law, Two: supremacy of the constitution, Three, separation of powers. We have seen there is so much confusion of powers between the legislature, judiciary and the executive.

Cultural heritage should be reflected in the constitution. Therefore in this regard we need the local court and this local court should be established in the local levels, and the people who are manning the local courts should be financed by the state. The

above directive principles therefore should be enforceable in law.

Three, constitutional supremacy. The constitution to allow the Parliament to amend any part of the constitution by 75% majority vote. The Parliament's power to amend the constitution should be limited. This case there should be a section that cannot be amended by the Parliament, for example, the land referendum. The public therefore should be involved in the referendum and the amending of the constitution and that is why we have the people participating in the constitutional review process and the people who are legitimate are the NGO's and judges, to guide in the constitutional review process.

Four, we have citizenship: All gazetted Kenyan citizens become automatic citizens of Kenya, that is the 42 tribes. A Kenyan should acquire citizenship by birth, registration, and naturalism only. A child born of one Kenyan parent regardless of parent gender should be entitled to citizenship after meriting special conditions and in this case we don't have people who are coming for their malicious affairs, to marry our daughter only to bring us confusion. The right and obligation of a citizen, and the right of expression, freedom, security and politics, and all citizens must have equal rights. The people should have one citizenship. There is no dual citizenship. The documents that Kenyans should carry as an evidence of citizenship are birth certificate and identity cards.

Five, defense and national security: The discipline forces, the military and the Para-military police, prisons and so on to be established by the elected commission and the Parliament. The commission should be used to discipline the armed force. The President should remain the Commander in Chief of the Armed Forces, and the power of the executive to declare war should be very limited for example, us the Pokot we have been having a problem with our Para-military personnel. The power of the executive to declare war should be limited. The Parliament should permit the use of extra-ordinary powers in emergency cases in war in national disasters. In selection and breakdown of public order. The President should have the authority to invoke these emergency powers. The Parliament remains the chief organ to solve the emergency cases.

Political parties: Political parties should sensitize the citizenship of their rights through their manifesto's and development. The constitution to assist on the formation of governance, or norms and leadership as long as it remains independent. The number of political parties to be limited to five only. The political parties to be financed by their own members, and well-wishers but not the public resources and the public funds should not be used by any political party. Political parties should depend on their own funds apart from Parliamentary elections, and these elections must be free and fair.

The structures and systems of government: I am of the view that we retain the Presidential system of the government. We also adopt the Parliamentary system of government in which the Prime Minister is appointed from the majority party in Parliament and the President remains more or less ceremonial. The President will implement policies and not to decide and also sign other international affairs and correspondence after deliberations from the Parliament.

The Prime Minister: According to their merits, qualifications, and credentials, we don't want to have a confusion where somebody is put in a place where he or she cannot merit. There should be no coalition of government. The power to be given to Parliament. We should have unitary type of government but the affairs of the state to be centralized to the district level. This calls for more powers to be given to the local authorities.

Eight, the legislature: 75% nomination should be vetted by Parliament, and the Parliament should be given all the powers in any state undertaking. The powers given to the Parliament should not override the constitution. The Parliament should set four months per year to meet the people, and the other days to be at the Parliament. This calls for the Parliamentarians therefore to have their offices. We don't want the MP's to take the offices to their homes. We want them to centralize their offices where the people can meet them, and should call for exactly four months. There should be no changes to be made to every requirement for voting and contesting Parliamentary, so it should remain as it is. All Parliamentary contestants should be graduates because we are in a new millennium. We should introduce moral and ethical qualification for Parliamentary candidates. The people should have a right to recall their MP when he or she has not delivered the services required. The MPs therefore should act on the basis of conscience, conviction, and instructions from the constituents or parties. So they should act as per our instructions, but not another instructor coming to confuse the whole system. The constitution to establish a commission to determine the salaries and benefits of members of Parliament but not the currently event where by they are vetting their own salaries, disregarding what the public is getting.

The concept of nominated MP's should be based on those who are mostly the marginalized communities, and persons with disabilities, including gender as an affirmative action. The constitution therefore should for a minimum of 40% women in the legislature as well as in local authorities, and the constitution should govern the conduct of the Parliamentarians in a multi-party state. This therefore, we should have one chamber of Parliament. Parliament powers to remove the executive through a vote of no-confidence should be adequate. The President shouldn't have the powers to veto legislation passed by Parliament but the Parliament should remain supreme in power. The legislature should have the power to override the President's veto in case of emergencies, and the President should have the powers to dissolve Parliament during election campaign. We should not stagger election for Parliament so that there is time when there is no seating Mps.

Nine, the executive: The constitution should specify qualification for Presidential candidates. The Presidential candidate should be a graduate and not a member of Parliament, and not a member of any party. The President's tenure should be fixed to one term of five years, and the functions of the President to be defined in the constitution such as ceremonial implementation, and signing of international affairs and the constitution should set limits of the Presidential powers.

Com. Lethome: (Not clear)

Mary Chelengole: The judiciary: In the judiciary we only want to establish the traditional court, whereby they should exercise

full judicial powers and they should be funded by the state. In the local government, the mayors and the councillors should be elected directly by the people and the mayors and the council chairmen should serve in 5 years, and these people should be independent from the government.

The electoral system should remain. We should practice the current representation of the electoral system, and lastly we have got the basic rights. Where we need the basic rights to education, we need also power, we need infrastructure, because you cannot move from one place to another, security, health care facilities, and also shelter. To windup, all of them we should also remove the excessive domestic violence that we have in our homes, so that we have got no forceful wives inheritance, female genital mutilation, and even rape, and including rape within marriage. Thank you.

Com. Lethome: Do you have any question. Mary one question. You said, sit, just have a sit, remain in your sit. You said some cultural practices should be banned, like forceful wife inheritance. Why did you use the word forceful. Okay, I want you to elaborate on that. Number 2, you were talking about domestic violence, what do you recommend to be the punishment of a husband who batters his wife?

Mary Chelengole: I talked about the constitution should get rid of harmful traditional practices like the female genital mutilation. We have got also forced wife inheritance because you find that some women who have not delivered even a child, and they still want to go ahead. that is not forced, that is a personal decision. Also what I said about domestic violence in case of maybe a husband battering his wife, there should be a law to protect the women, and these men should (interjection).

Com. Lethome: Do we use traditional law or the contemporary law? Akiletwa kortini ya siku hizi au ile ya kimila?

Mary Chelengole: We go to the traditional court.

Com. Lethome: Okay asante. Tuendeleo, Jacob Longarani na yule mkulima yuko wapi?

Jacob Longarani: Ndio Bwana Commissioner, nilikuwa na jambo moja tu ya kwamba kuna taabu moja katika serikali yetu ya Kenya. Yaani watu wakubwa kama sisi ambao ni karibu kustaafu, nataka kwenda ku-retire, kupata pesa ya retirement ni shida. Kwa nini serikali hapana shikilia saa ile mtu ana-retire anaingia mara moja hapo in fact tumezoea pesa. Kwa hivyo kila mtu katika kuondoa namna hio napata haki yake haraka, haraka namna hio, yangu namna hio. (laughter).

Com. Lethome: Asante sana mzee. Haya tuendeleeni, kuna Jacob mwingine sasa, Jacob Petare?

Jacob Petare: Yangu ni shukrani kwa ma-commissioner ambao wamekuja hapa West Pokot, kwa sababu tangu tupate uhuru hatujawahi kuona kitu kama hii tangu zamani, na Wapokot walikuwa wanasauliwa. Yangu tu itakuwa ni machache.

Ya kwanza: Wapokot wenyewe wana sheria zao ambazo tungeomba Katiba ya Kenya iheshimu sheria ya Wapokot wenyewe ambayo wameunda tangu zamani. Tungeomba Katiba iheshimu moja, yaani kwa mfano, mtu akiua mtu kuna fine ambayo Wapokot walitunga tangu zamani. Hio sasa tungeomba Katiba ya Kenya iandikwe ili hata mtu akiuawa, Mombasa, fine itakuwa namna hiyo, na local courts ya Pokot yaani kortini ya Wapokot. Katiba ya Kenya iheshimu, kwa sababu huwa wanafanya mambo yao na wanamaliza huko nyumbani. Nyingine kama kuiba na mambo mengine. Haya, sheria ya Wapokot, kama, tunaomba kama Wapokot tunataka serikali ya majimbo kwa sababu sheria ya Wapokot hailingani na sheria ya wengine. Sasa mtu akiishi hapa West Pokot na anaona haingiani na sheria ya Wapokot anahamia mahali pengine ama?

Com. Lethome: Unataka iwe kwa mkoa, ama iwe kwa district, ama kwa constituency?

Jacob Petare: Iwe kwa district.

Com. Lethome: Kwa hivyo kila district iwe ni jimbo moja?

Jacob Petare: Ni jimba moja.

Com. Lethome: Kwa hivyo Kenya tutakuwa na majimbo sabini na nne?

Jacob Petare: Jambo lingine, tungeomba kwa West Pokot tugawiwe constituency, kama mbili ya Lalena Lelan, kwa sababu Lelani ni nchi baridi sana.. Ukienda kuangalia Lelani ni 15 degree Centigrade, na sehemu za Sigor mahali ya ofisi yetu ya constituency saa hii, it is 30 degree centigrade ambapo ni mbaya sana mtu akitaka hapa Lelan aende huko pengine hatapona. Ukienda kuangalia Sigor is 700 above sea level and Lelan it is over 3,000 above sea level, na mtu akienda huko sasa inakuwa ni vibaya sana. Sasa tungeomba sehemu za Lelan igawiwe constituency yake peke yake na ijifanyie mambo yake.

Haya lingine, tunataka constituency, yaani offisi ya constituency ambapo mbunge atakuwa mkubwa hapo. Halafu hio offisi iwe na nguvu kama yeye iko kwa ofisi ya DC saa hizi ambayo pesa zote zinatoka kwa serikali, Central Government, wanakuja kwa DC, sasa badala kwenda kwa DC inakuja kwa ofisi ya MP, halafu akitumia hizo pesa zetu kwa njia mbaya tunatoa yeye baada ya miaka tano, kwa sababu hata DC

Com. Lethome: Hautaki kutoa yeye katikati mpaka miaka tano?

Jacob Petare: Hata wakati wote tunaweza kutoa yeye akiwe mbaya (laughter). Kwa sababu pesa zote zikitoka huko kwa Central Government zikuje kwa DC zinaweza kuhamishwa. Kama DC anatoka Mombasa anaweza kuhamisha mpaka Mombasa, kwa sababu hajui shida ya West Pokot.

lingine, DC awe security officer pekee yake katika district. Hakuna kazi ingine ambayo anabaena, anabaena kama security officer. Na madiwani, madiwani walipwe na Central Government, pesa zitoke kwa Central Government, kwa sababu wamechaguliwa kwenda huko kwenda kumaliza mali yao, yenye wanapeleka kutoka nyumbani. wanachaguliwa, kufika huko wanakuja kuuza ngombe yote na kwenda kupeleka huko kwenda mchango na kufanya mambo mengine, kwa sababu hao watu wameanza kuwa maskini kuliko mbeleni.

Haya, President awe chini ya sheria, kwa sababu kila kitu ambacho unaona Kenya hii mambo ya ufidadi. Ufidadi umetokana kwa sababu President ako juu ya sheria. Anaweza chukua chochote anachopeda, na anapea mwingine mwenye anafuata. Sasa mtu akipelekwa kortini mtu yoyote mwenye amekuwa mfidadi sasa huyo judge mwenge ana deal na hio kesi sasa atambiwa ati fungua hio kesi ili asifutwe. Kwa hivyo huyo mtu awe chini ya sheria, ili hata sheria i-deal naye.

lingine katika hii area ya Lelan naitwa catchments regions, karibu na kuwa source of water ya kila mahali. Maji inatoka hapa nakwenda mpaka Lake Victoria, na kutoka hapa mpaka lake Turkana. Tungeomba serikali watupatia msaada ili tuchunge area hii. Wasipo tupatia msaada ili tuchunge the sources of water, tunaweza kufika msitu yote mpaka nchi ikauke. Lakini hatuwezi kubali namna hio, hatuwezi kubali. Tunataka tupatiwe msada fulani ili tuchunge kabisa na sisi wenyeji wa area tuwe wa kuchunga area. Haya chiefs and assistant chiefs wapigwe transfer. Mtu anadiwa na kwenda transfer kamamwalimu ama kama mfanyakazi wa serikali yoyote kwa sababu mtu akiweza kukosana na chief hio kukosana itakaa mpaka huo mtu aende retire.

Com. Lethome: Kisasi.

Jacob Petare: Kisasi (laughter) kwa hivyo huyo, huyo mtu aende transfer mwingine akuje. Haya, trust land ile inayosimamiwa na county council itupiliwe mbali. Mtu binafsi asimamie area yake, mtu binansi Haya, minerals, itatakikana kusimamiwa na citizen yaani mwenye shamba akisaidiwa na county of the area. County kwa mfano, county of Pokot, county of the area, anasimamiwa na mwenye wa area na county. Inginge tungependa Katiba iweke elimu ya bure, free education. Especially sisi watu wa kuhama hama, watu wa kuchunga ngombe, kwa sababu wanaweza kuhamia hapa na kuhamia mahali pengine sasa wanajenga schools, boarding schools ili waishi huko, watoto waende huko, halafu watu wahame na ngombe zao. Halafu, free medicine, yaani wanatoa dawa ya bure kwa ma-hospitali. Inginge ni ya mwisho ni ile inaitwa re-appointment. Mtu akitolewa kwa kazi, pengine anatolewa kwa makosa hakuna haja ya kwenda kurudiwa tena kupigwa transfer kwenda kazi ingine. Mtu kama ametolewa, ametolewa kabisa kama alikosa kwa nini anaenda mahali pengine? Kama aliharibu hapa si ataenda kuharibu mahali pengine. kwa hivyo huyo mtu aende na yule mtu ameenda retire anatakiwa kwenda kulisha wajukuu nyumbani sio kwenda kufanya kazi tena. Asanteni.

Com. Lethome: Asante sana. Sasa tupate mama Veronica Samuel, mama kuja ni zamu yako sasa. Nilikwambia tuta-balance upande wote.

Veronica Samuel: Nyono nyuu Veronica Samuel,

Translator: Anatoa shukrani.

Com. Lethome: Toa sauti mama, anza na jina lako.

Veronica Samuel: Jina langu ni veronica Samuel (Kipokot).

Translator: Anasema shukrani

Veronica Samuel: Soro nyo wou

Translator: kwa siku hii ya leo.

Veronica Samuel: Kugh nyo komiitan omwoghoy

Translator: Kile kitu anasema maoni yake,

Veronica Samuel: Ngolyondee nyaan kuu

Translator: katika Katiba hii ya Pokot.

Veronica Samuel: Ompo katiba Pokot

Translator: Anasema mambo ya kortini iweko na local court ya area ya wazee.

Veronica Samuel: Kmoo cheecha kumpuur ngalecha kusiir kepa kotiini nyopo Sooch

Translator: kwa sababu mambo isikimbishwe speed iende kortini kubwa.

Veronica Samuel: Ompo wolo mii kirupteghoto ompo kotiniin

Translator: Kwa sababu wa mama waliposikia wengine.

Veronica Samuel: Ato otini kiluum yotuuno walaka,

Translator: Kwa sababu wamama wengine walifurahia ya kwamba hii Katiba ni pengine itawasaidia wakimbize mambo yao kortini lakini si vizuri kwa mila ya Pokot.

Veronica Samuel: Kuchaam piich nyoman ompo wolo katiba nyopo Pokot kuu kungorochoy piich

Translator: Hana mengi sasa.

Veronica Samuel: Nyoo moo tungon nyee ngaal choo chang

Translator: Asante.

Com. Lithome: Asante Mama Veronica. tupate mama mwingine, Cheptotunyang Lokolkore, njoo mama.

Cheptotunyang: Soro nyo wou Veronica. Nyono yotoo anga ngalana.

Translator: Anaitwa Cheptotunyang.

Cheptotunyang: Kurenanuun Chepotuunyany

Translator: Lokolkone

Cheptotunyang: Lokolingole

Translator: Shukrani kubwa,

Cheptotunyang: Soro nyo wou paat

Translator: kwa sababu amefika hapa,

Cheptotunyang: Ompo wolo kiy kereluu chaa yeteyii

Translator: Nataka kutoa maoni yangu sasa.

Cheptotunyang: Ompo wolo ko tomanyee keluumachaa nyee tagh

Translator: Sababu mambo kama haya hajapata siku ingine kuona.

Cheptotunyang: Ompo acha yotuun, mwoghechaa lo soro nyo wou

Translator: Kama wamama,

Cheptotunyang: Ompo wolo yotuun tyaa

Translator: tunashkrani sana,

Cheptotunyang: Ktuungo chaa soro

Translator: kwa sababu hawa ni walevi.

Cheptotunyang: Ompo wolo kiluuki papootuno tomasiis po kumuun wey.

Translator: Maoni yale nataka kutoa,

Cheptotunyang: Kinonuut yee nyan kugh,

Translator: hatuwezi kusomesha watoto.

Cheptotunyang: Mo kimuchee cha nyee kesomeshan monung

Translator: kwa sababu wamama ziadi,

Cheptotunyang: Ompo wolo yotuun choo chang

Translator: ambapo kama wangukuwa na uwezo wangeweza kusomesha watoto.

Cheptotunyang: Nyo to'kotuung yootuno owesyo to kuusomeshonoy monuung

Translator: Nasema sasa wazee wamepotea.

Cheptotunyang: Nyo k'mwoghecha loo kikutotyoo papootuno

Translator: Kwa sababu wanawacha jukumu yote ya kusomesha watoto hata kulea kwa wamama.

Cheptotunyang: Ompo wolo kopuustoo ngalee lowur hata chopo kisomeshonot onguut

Translator: Sasa wameshindwa na mambo ya masomo

Com. Lethome: Mwambie anapenda mambo ya masomo iende namna gani ndio kina mama wafaidike.

Translator: Mchiini kegh nee ompo ngale cheete nyaa po pooy?

Cheptotunyang: Ki'kupol chanee wolo ngarekee yee nyuu cha nee.

Translator: Naaka watoto wasomeshwe bure.

Com. Lethome: Ngoja, itakuwa rahisi, situlikubaliana? Nitatoa red card. Kila mtu aachiwe atoe maoni yake, unajua hio tunaweza kusema ni madharau kwa sababu ni mama ndio mnapiga makelele, mama endelea, amesema masomo ya bure?

Translator: Masomo ya bure.

Com. Lethome: Nao wazee ambao wanakataa kusaidiana na akina mama kusomesha watoto unataka sheria iwachukulie hatua gani?

Cheptotunyang: Kemokenyii loo kighoy lo nee poyii chuu katagh kusomeshan monuungee nyaa?

Translator: Basi tunashukuru sasa kwa sababu,

Com. Lethome: hilo swali nimeuliza...

Cheptotunyang: Kateepan tepuutyoon ndoo noni.

Translator: Ameulisa hiyo swali

Cheptotunyang: Omochan paat kee ngolonchuu

Translator: Anataka ya kwamba wazee hawa wazungumziwe tu.

Com. Lethome: wasichukuliwe hatua? Haya, Nicodemus amoywal.

Nicodemus: Asante sana, kwa majina naitwa Nicodemus Moywal. Mimi hapa niko na memorandum na yale nitaongea nitapitia juu. Kwanza kabisa ningetoa shukrani zangu kwa nyinyi ma-commissioners ambao mumetutembelea hapa kwa sababu mara kwa mara tulikuwa tunasikia muko Nairobi. Lakini kama mumetutembelea hapa mimi natoa shukrani.

Ya kwanza nikuhusu mambo ya local authorities yaani serikali ya wilaya. Kwa maoni yangu mimi naonelea a kwamba, local authority ipewe jukumu la kuangalia maendelea zote ambazo zinafanyika katika wilaya yetu hii ya Pokot. Na pia wapewe jukumu ya kuangalia mambo ya raslimali yetu. Yaani Pokot County wapewe jukumu ya kuangalia raslimali zote ambazo ziko katika wilaya hii ya Pokot, na pia wapewe uwezo kama vile C.C. ako na uwezo. Ile uwezo wa DC, wapewe Pokot country.

La pili ni kuhusu elimu: Kabisa sisi Wapokot tulibaki nyuma sana tangu tupate uhuru mpaka sa hizi, sasa tunaonelea ya kwamba elimu kwa Kenya iwe ni ya bure ya lazima kwanzia darasa la kwanza hadi kidato cha nne. Halafu chuo kikuu iwe jukumu ya serikali kuangalia mikopo ya kupe wale wanafunzi wamefaulu.

Ya tatu ni kuhusu raslimali: Hapa hivi nikiwa hapa Lelan ile raslimali tuko naye karibu nayo sana ni msitu. Ninaonelea ya kwamba huu msitu upewe mkono ya wananchi waliokaribu na hapo, kwa sababu hao wenyewe ndio wanaelewa maana ya hio msitu. Sasa ingekuwa jukumu lao wapewe, wachunge wenyewe, kwa sababu tumekuja kungundua ya kwamba wale watu walipewa jukumu ya kuchunga hio msitu, hao ndio wale walaji kabisa. Kama ni kukata mbao, ni kuchoma makaa, hao ndio wako nambari la kwanza. Kwa hivyo sasa misitu yote iwekwe kwa mikono ya wananchi walioko karibu na hapo.

Kuhusu wanyama wa pori: Naonelea kwamba mnyama wa pori akileta madhara yoyote, kwa mfano akileta kupe, akiuma mtu, ni jukumu ya hio wizara iangalie huyo mtu na kupewa malipo, apewe compensation, kwa ile damage ambaye apewe na yule mnyama, na pia ile raslimali itatoka kwa wanyama wa pori, wagawiwe wale wenyeji wako karibu na hapo ili wapate pia kufaidika.

La tano, ni kuhusu mambo ya afya. Ninaonelea kwamba iwe jukumu la serikali. Hi Katiba itabue kwamba sisi wana Kenya tupewe dawa ya bure. Kuanzia hospitali za zahanati dogo mpaka national hospital. Na iwe kwamba madaktari, doctors iwe rationing. Wapewe kila, at least kila wilaya wawe na ration ya ma-doctor, kwa sababu hapa zaidi tuko na madaktari wale watu wameenda nursing, na pengine clinical officers pekee yake, lakini hatuna doctors. Iwe kwamba kila division, iwe na doctor ambaye anasimamia kila division.

Halafu, na mambo ya kilimo yaani, agriculture, iwe ni kwamba iwe ni jukumu ya serikali kupea wananchi fedha ya kusaidiana naye. Wapewe loan, kidogo ili waweze kuendelea mambo ya kilimo. Na iwe pia jukumu ya serikali ya kuangalia soko kwa sababu kwa sisi hapa tuko na shida sana kwa hali ya soko ya kila aina ya mimea hata pia. Kwa mfano hapa tuko na shida ya soko ya manyoya ya kondoo na hapa tuna manyoya ya kutosha. Lakini hatuna. Na hiyo saa mnyama, kondoo hakuna soko, haina maana yoyote. Sasa iwe jukumu la serikali kuangalia soko kabisa.

Na la mwisho, si la mwisho, kwa sisi wale wafugaji wa kuhamahama, tungeonelea kwamba hii Katiba iangalie wale watu wa kuhamahama. Wapewe commissioner, nao pia wawe na waziri wa kuangalia masilahi yao.

Halafu la saba, kwa sisi, naongea kwa jukumu la vijana, kwa sisi hapa. Vijana wa siku hizi tumesoma lakini hatuoni serikali ikijali sisi kutafutia sisi kazi. Ndio unaona wanalalamika kusema kuwa vijana wanakuwa chokora, wanaenda mpaka wanakula dawa ya kulevya. Sio kwa kupenda kwao, kwa sababu ya kukosa namna. Mtu hana namna hana kazi, amesoma, kazi ya mzazi ni kufukuza hawa anamwambia umemaliza ngombe. Iwe ni jukumu la serikali kuangalia kazi y akila Mkenya, yule mtu amehitimu shule.

Na la mwisho, tuwe na kortini ya kienyeji ambaye itaangalia masilahi, ama iangalie mambo yetu kama Wapokot. Tuwe na customary law ambaye itaangalia mambo yetu ya Pokot. Kwa hayo machache nasema asanteni.

Com. Lethome: Asante sana Nicodemus. Tupate Emmanuel Kariki, ebu ngoja. Hiyo mashini iko sawa? Can you test it now? Put it on, you are Emmanuel? Say your name na uendele.

Emmanuel Kariki: Jina langu naitwa Emmanuel Kariki. Nina mambo matano hapa ningependa niseme, halafu nitatoa hii memorandum. Kwanza ni kuhusu trust land.

Tumeona neno trust land liweze kutupiliwa mbali kwa sababu mtu mwingine asiweze ku-kusimamia kwa shamba lako. Kwa hivyo kuwe na registered community land instead of trust land.

La pili: Ningependelea katika new constitution hii tuwe na Truth and Justice Commission ambayo itaangalia kuhusu claims ya traditional lands, na shamba ambayo wazungu walichukua. Kama sisi hapa katika sehemu yetu hii tungeonelea pia kuwa kulikuwa na boundaries ya zamani ambayo labda ingesaidia sisi kwa kodi, ama mambo mengine katika wilaya hii. Kulikuwa na mpaka wetu unatoka Moeben River, Jamrukoe, Nai River, Kamasha, Chorwa, Kabiako Kamla Kon. Hio boundary iwe maintained na hatujasema mtu aondoke. Lakini tunasema ili tuweze kupata kodi zaidi ama tuwe na raslimali ambaye iko sehemu hio ambayo itafaidi sehemu yetu hii ya Pokot na labda tutaweza kuendelea zaidi.

Pili: Natural resources, ningesema county ama district jinsi tunavyo hata wakati huu kuwa asili mia themanini ya income ambayo tunapata kwa natural resources ibaki kwa county. Halafu asilimia ishirini iende kwa Central Government. Pia tungetaka kwa, yule ambaye tunamuita clerk, lakini tungependekeza kuwa awe county manager, aweze ku-prepare budge kila mwaka ambayo watatusomea income ya, ambayo imetoa natural resources ambaye itafaidi jamii, ili tujue pesa ambazo tutakuwa tumepata iweze kutufaidi kwa maendeleo ambayo tunayo. Pia kuna shamba ambalo, labda tumepeana kwa kusaidia nchi nzima, kama ile ya Turkwel Gorge. Jamii yetu ipewe compensation, na lazima wafuate pia present market price ya ku-compensate hao wananchi ili, kwa sababu jamii yote itakuwa imefaidika. ama niki-lease iwe ni karibu miaka ishirini hivi, halafu wajue ni kitu gani baada ya hayo.

Kwa local government, tungeonelea kuwa, county iweze kupata pesa kutoka kwa treasury. Halafu, nimeandika kwa kizungu wacha nisema hapa. Each county will receive from the treasury its annual budget that will designate how much has been set aside for the different sectors and departments. The local authority will also have powers to raise its own taxes. Kwa hivyo hizo pesa ambazo tutakuwa tumepata budget kutoka kwa treasury, tuweze kuua hii itaenda sehemu gani katika wilaya, kwa sababu tutakuwa tumepata hio budget. Na tunganese pia mwenyekiti wa county, aweze kuchaguliwa direct na electorate na wenyeji. Kuliko wakati huu ambapo ma-councillors wanaenda kukatana na ku-elect chairman ambaye sisi kwa maoni yetu tungeona yeye angefaa, na lazima akae miaka mitano. Kwa mwenye kiti ningependelea kuwa awe na elimu ya 3rd level qualification. I mean 3rd level qualification, awe amemaliza either chuo kikuu ama amemaliza form 4, halafu awe amefanya training fulani kwa chairman. Na pia ningependekeza kuwa councillors waweze kupwewa mishahara ya kati ya elfu thelathini mpaka elfu hamsini. Ili waweze kujitosheleza na waweze kutusaidia pia, na tungeonelea kuwa hao ni wengi wakati huu. Wawe watu karibu kumi katika constituency, councillors watu kumi.

Basi nikienda kwa judiciary: Ningependelea kuwa, tumekuwa na matatizo mengi kuhusu judiciary. Kwa hivyo ningependelea tuwe na customary courts ya Pokot community ambayo itaangalia maslahi ya mambo madogo, minor cases and also permit to mete out their own approved form of punishment. Ili pia wajue kama mtu amefanya makosa haya, punishment gani itafaa kwa huo mtu. Tunganese pia kama ni dispute ni baina ya Pokot na non-Pokot waweze ku kubaliana. Iwe ni customary courts ama iwe ni ile ya kawaida. Kama ni kati ya Pokot na yule ambaye si Mpokot. Na tunganese pia kwa customary courts tuwe na stages kuanzia chini mpaka juu. Tungekuwa na “Korkorpoi” 1 (one) ambaye itaanzia kwa sub-location “Korkorpoi”2 (two), halafu pia iende kwa district tribunal. Ili hio stages ambayo nimesema kwa customary laws, kuwe na stages pia ambayo wataanzia from the bottom. Tuwe na “Korkorpoi” 1 (one), “Korkorpoi” 2 (two) halafu district tribunal. Ili waweze kumaliza, kama inaweza kumalizika katika kiwango cha chini waweze kutatua kuliko liwachwe tu liende mpaka district tribunal. Na district tribunal i-constitute watu tisa, iwe na watu tisa, na hao watatu tisa watu watoke kila constituency kwa sababu wakati huu tuna constituencies tatu. Kwa hivyo wakitoka tatu, tatu hatutakua tumekuwa biased kwa distribution yetu ya district tribunal committee na tuseme pia mmoja kati ya watu tisa, mmoja awe retired civil servant ambaye atakuwa karani ama clerk, ambao tunamuita “Kirkirm”. Halafu pia mwenye kiti ambaye tunamwita "Arimot" na hao wata-fix calendar hao, watajua wakati gani watafanya kesi, wakati gani. Na clerk ama mwandishi pamoja na mwenye kiti lazima wawe wamekuwa na miaka hamsini na

tano na zaidi, kwa sababu ni wazee. Ndiposa tunasema elders, lazima wawe wazee. Pia wakati kuna mabishano, they will also administer Pokot oaths ambaye tunaita “Muma”. kwa hivyo hawa wazee tisa watapewa jukumu hilo pia ya ku-administer Pokot oaths. Lakini tutakuwa na Judicial Service Commission ambayo wata-provide funds kwa customary courts and they will also oversee their activities. Itakuwa pia jukumu lao pia kwa Judicial Service Commission kuangalia kazi ambayo wale wanafanya.

Kwa Bill of Rights: Tungeonelea kuwa bill of rights katika sheria yetu hii ya wakati huu iwekwe katika chapter ya kwanza, kwa sababu bill of rights ni kitu muhimu kwa mwanadamu sana, kwa hivyo katika constitution yetu tungeonela kuwa iyo iwe katika Chapter One.

Kwa elimu tungenesema, elimu iwe ni ya bure na ni lazima ya primary education. Free and compulsory primary education. Ningependekeza pia msimu wa elimu ya

8-4-4 utupiliwe mbali, na tuwe na ile ya zamani ya 7-4-2-3 system. Tunaona hapo itakuwa ni vizuri kwa sababu nikama kichungi ambao tutapata watu ambao wanafika vyuo vikuu kama watakuwa wamehitimu vilivyo. Pia tungetaka constitution itupatia guarantee ya equitable distribution of teachers, yaani tuwe na waalimu sawa, raslimali tertiary facilities schools throughout the republic. Yaani tungepedekeza kuwa lazima serikali tukiandika constitution yetu hii, tuwe na equitable distribution of teachers, resources, tertiary facilities and schools throughout the republic.

Karibu na mwisho kuwe na affirmative action programme ya kusaidia historically disadvantaged groups, kama wamama ama wanawake, youth, pastoralist, disabled, street children, squatters, slum dwellers, Pokots and Turkanas. Tumeona kuwa jamii wengi walibaki nyuma kwa sababu kama district yetu hii ilikuwa inaitwa closed district. Kwa hivyo mambo mengi hayakutufikia. Kwa hivyo tungeonelea kuwe na affirmative action ambao inaweza kusaidia sisi Wapokot, na Waturkana, na wale wamama, na wale wengine ambao hawakubahatika katika jamii, kwanzia wakati wa ukoloni. Na pia the programme will protect and promote the disadvantaged groups in terms of employment services and infrastructures. The affirmative action programme should last for a period of time. At least tume-propose miaka kumi na tano. Tukipewa miaka kumi na tano, bila shaka tutakuwa tumefika par na wale wengine, na bila shaka tutaweza ku-compete favourably na wale wengine. Asante sana.

Com. Lethome: Asante sana Bwana Emmanuel. Sasa tunazungumza habari ya equality na affirmative action. Ngoja tumpe mama sasa. Josephine James, anza kwa majina mama, jina.

Josephine James: Kuree nanuun Josphine James

Translator: Anaitwa Josephine James.

Josephine James: Otungoon tukuun odeny paat kule

Translator: Ana mambo mawili.

Josephine James: Oyokuunan soro ompo akwa choo kamuukakwa to oreelu

Translator: Anarudisha shukrani kwa nyinyi kufika hapa.

Josephine James: Ata mukaakwa ta angaraa keecha

Translator: Ili mtusadie kutoa maoni yetu.

Josephine James: Takemwaghacha konuut koo chaa

Translator: Kama wamama.

Josephine James: Otoghonan maoni lee yoo

Translator: Natoa maoni kama mama.

Josephine James: Kuhusu Monung.

Translator: Kuhusu watoto.

Josephine James: Ompo Ngale monung

Translator: Kuna wamama ambao wamebaki manyumbani.

Josephine James: Miiteni Yootuno chiini kikuudong keeston

Translator: na watoto wao,

Josephine James: Nkoo monuungekwa

Translator: na hakuna mtu anaweza kuwasaidia,

Josephine James: ak momiinye chii nyo kengaraak

Translator: kwa masomo.

Josephine James: Ompo lenye masomeengwaa

Translator: Wakati pia baba pia alizaa watoto wake,

Josephine James: Otinii kiyiy chii nyole papoo monuungechii

Translator: na akawaacha watoto wake hajasomesha,

Josephine James: Kpuusto monuunge chii mokuu someshaan nyee

Translator: Sasa mama hawezi kusomesha,

Josephine James: Nyo memukoy nyee nyuu yoo tokusomeshan

Translator: Anaweza kushomesha mmoja.

Josephine James: Mukoy kusomesha akongaa

Translator: Lakini wengine hawawezi,

Josphine James: Wolo meloo lowur

Translator: Kwa hivyo nasema,

Josphine James: Nyo yee nyuu

Translator: wataka elimu ya bure.

Josphine James: Angarakeecha ompo elimu

Translator: Kupatana na watoto,

Josphine James: Kruupategha ngat ompo ngala monuung

Translator: kuna watoto ambao wanawezapata mali.

Josphine James: Miito monuungo cho mukoy kunyoruu malii

Translator: Na kuna wengine watapata mali imekwisha.

Josphine James: Nko walaka choo monyoruu nyee malii

Translator: Kwa hivyo tunataka watoto wasaidiwe,

Josphine James: Karaam kengaraak nyuu to knyooru mali chii

Translator: Kwa walimu ili wapate mali zake.

Translator: Kuna pia, kuhusu watoto wasichana.

Josphine James: Mitooni monuungo chole tiipin

Translator: Hawana haki ya kumiliki mali kwa Wapokot.

Josphine James: Mo choghchuniinyee Pokotuu mali

Translator: Wasichana wapate elimu kwani wasipopata.

Josphine James: Mchiini kunyoru malii kwaa

Translator: Sasa atakuwa ili mtu amepotea na atakuwa bure tu na,

Com. Lethome: Asema chokora

Translator: Na atakuwa chokora.

Com. Lethome: Sema hivyo.

Josphine James: Mwagha lee nyiini

Translator: Wakati wa zamani Pokot,

Josphine James: Atay kilee kony

Translator: Mtu alikuwa anaoa wanawake watano,

Josphine James: Kii yipoy chii koor chole muut

Translator: Lakini sasa ni mmoja.

Josphine James: Lakini yee ki keep akonga

Translator: Sasa mtoto huyo atapotea tu namna hiyo

Josphine James: Dongoy nyuu monuungoona ku-pototoy

Com. Lethome: Hio kuhusu watu kuo napendekeza nini? Wazee wambiwe waoe watano ama nana gani? Anapendekeza vipi? (laughter)

Translator: Imwoghenyii lo nee nyaa?

Josphine James: Omochaan kwiip akonga

Translator: Anaonelea mzee aoe mwanamke mmoja.

Josphine James: Lakini, ongorokweecha nee monuunge chuu dongoy

Translator: Na sasa anaomba usaidizi kwa wale watoto wanabaki.

Translator: Kuhusu wasichana tena.

Josphine James: Ompo ngala tiipin kungat,

Translator: Anataka wasichana wapewe haki kama wengine, mali,

Josphine James: Omochan kechogh chuu malii kwaa

Translator: kwa sababu Wapokot,

Josphine James: Ompo wolo ngetoy Pokotuu

Translator: Anapatia wavulana, hata anaweza katia shamba, plot, hata na kupatia ngombe,

Josphine James: Choghchiini karachuuna ompuun hata plootiin

Translator: na anawacha wasichana.

Josphine James: kudong cheptoo

Translator: Kwa maoni yake sasa,

Josphine James: Ompo maoninyaan,

Translator: anataka hata msichana pia apate haki hiyo.

Josphine James: Omochan keetoo cheptoo mali tukwil

Translator: Apewe pia ile apate kujisaidia naye.

Josphine James: Takungarakaa kegh

Translator: Ili naye aweze kulisha naye watoto wake.

Josphine James: Ata kupaghaa tikwil chechii monuunge

Translator: Kwa sasa ni hayo.

Com. Lethome: Asante Mama. Pande hii mama, asante kwa maoni yako. Kama tulivyosikizana pale mwanzo, ikiwa mama amewa-provoke kwa hayo maoni yake, mtu mwenye maoni tofauti na hio atakuja atatowa hapa hivi. Haya tupate Samuel Kudoki.

Com. Lethome: Mtuu mwenyee maoni tofauti atakuja kutoa hapa hivi. Haya tupate Samuel Kudoki.

Samuel: Eh asante sana. Mimi naitwa Samuel Kudoki. Maoni yangu ya kwanza ni mambo ya elimu ya bure kwanzia std one mpaka form four. Hiyo itatusaidia kwa sababu tulibaki kama closed district kwa wakatii wa ukoloni. Ya pili, ningeeomba serikali ya kwamba wamalize corruption, yaani ufiisadi ambaye imeletee mambo mabaya.

Ya tatu, ningeeomba serikali kupatia kila mtu cheti cha shamba (title deeds) kwa Pokot District. Na ipatikane katika District Headquarters kuliko kusafiki mbali kufatuta title deeds. Yaa nne, kuna mizozo mingi kati ya Pokot na majirani zao. Ningependa serekali kuangalia mipaka ambayo ilitengeneswa mwaka wa 1944 ili tuepukane na mizozo ya kulingana na majirani zetu.

Ya tatu, madiwani walipwe na Central Government kwa sababu sisi ni viongozi ambao wako karibu na wananchi, si vizuri wazilipwe mshahara.

Ya nne, kwa mambo ya sheria, sisi Wapokot tungependelea tuwe na wale wazee kutoka vijijini kuliko kupelewa kotini halafu wachunguze kezi ndogo ndogo kama mambo ya mashambaa, si vizuri tupeleke kotini na kezi kama ya kung'ang'ania ngombe ama mbuzi na civil cases. Tuwe na wazee wa kokwoo kutoka sub-location, halafu location na tribunal court.

Com. Lethome: Ni wazee na wamama au wazee pekee yao?

Samuel: Wazee wanaume pekee yao.

Ya sita tuko na institutions za serikali ambazo ziko katika District yetu hapa haswa hii nyanda ya juu highlands kama KTDA na Lake Basin. Tungependa hizo mashirika itusaidie sisi watu wa nyanda za juu. Kama vile tunahusika na mambo ya maji. Hizo mashirika itupandie miti, aforestation, kuzuia mmomonyoko wa udongo, na kupatia sisi hata loans ili tuchunge misitu vizuri na maji yaongezeke.

Ya nane, katika wilaya ya Pokot tuko na Turkwell Gorge, lakini Town zetu sote hazina mwangaza, tungependa serikali to supply kila Centre ili maendeleo yapatikane, kama shule ha hali kadhalika.

Ya tisa, mimi binafsi, ningeeunga mkono mambo ya kusongeza Parliament ili katiba iandikwa kamili tunapoingia katika Parliament

(uchaguzi) tuingie na katiba mpya. Halafu ya mwisho ambao ni ya kumi, sisi wakaaji wa West Pokot, uchumi wetu ni mifuugo. Tungependa serikali iweke KMC mahali karibu kama Kitale au Eldoret ili tupatee mahali karibu na kuz uia wizi na mambo mbali mbali. Kwa hayo machache, ninasema asante.

Com. Lethome: Tumpate sasa mama Mary Mwok.

Mama Mary: Kaineenyan kuree nanuun Mary Mwok.

Translator: Majiina ni hayo Mary Mwok

Mary: *Omwoghan loo soro ompo piichu kapka aswaneete. Ompowolo tomanyee kesuweecha asista anga. Nyo komwoghan paat ompo wolo mwoghu piich ngale kwaa ompo wono lenye, lenye ompo cha yootun, kmiitecha kesomeshonoy monuung. Omwoghan paat ompo okumpo pareen. Ompo wolo konyoy papootuuno kutogh title deed kainotuut kokwa atolapay kuwoo kwaltaa paranay kudong yootuno nko monung.*

Translator: Asante kwa watu wa tume ambao wamefika leo. Kwa sababu hatuja sikia maneno kama haya siku nyingine. Nimesema tu kwa sababu watu wamesema kwa mambo kama ya wamama ambao wanasomesha watoto. Kwangu mimi ningependa kuongea juu ya mashamba, kwa sababu wazee wanaandika majina zao pekee zao kwa title deeds halafu anaenda kuuza shamba watoto wabaki pure.

Mary: *Komwoghan lo, kekiirchuu yoo paar nko papoo. Tomowetoy kwoltoy papoo. Atootino mochoy kwaltoy keepa kengalal tukul. Ompo ngala tiipin cha kakiwaza kau, yonoy piich chole papotuun, komokan paat kechogh chuu paar werkoo nko tiipin kukarkegh. Nyo nyoni chichan.*

Translator: Ningependa tume hii iweze kuandikia title deed kwa jina la mama na baba na mama ili baba asiweze kuuza hiyo shamba. Kwa wasichana ambao wamedungwa miimba, wababa wana wafukuza, ningependelea tuu shamba zingawanywe kwao. Asante sana.

Com. Lethome: Ngoja mama, huyu mwenye kuweka msichana miimba, ungetaka adhabu yake iwe nini chini ya sheria?. Halafu lingine katika lile koti la wazee, ungetaka wamama pia wakae katika hiyo koti? (kokwoo pooy) haya hiyo mbili.

Mary: Chii chino kewos monuung nyo munuung kemokoy paat kenoni “fine”

Com. Lethome: Kama ngapi?

Mary: *Kusomeshan ato tomanyee kuwany skuul. Ompo kokwo, mchiini kmiiteni yootuno tukul takteer ngale chiino mwoghoy pooy ombowolo kaluku pooy ompuun melo reelu ngale choona kau ato kiito pooy ompuun.*

Translator: Kwa msichana, asomeshe kama hajamaaliza shule. Kwa koti ya wazee, wamama pia wawe ndani kwa sababu wazee hawa wezi kusema ni nini ilitokea kwa hiyo koti.

Com. Lethome: Samuel Achokop na kuna mzee ambaye alikuwa kwanza. Paul, are you ready now, after him eh.

Mwinjilisti Samuel Achokor: Nanina taka kutoa maoni yangu kwa ufupi. Kwanza ningependa kushukuru kwa nafasi hii kwa macommissioners wale ambao wamekubali kuja kusikiza maoni yetu. Pili ningependa kutoa maoni yangu kwa njia hii. Umaskini katika nchi ya Kenya. Katiba ingeweza kupuunguza na kuweka katika sheria ya kupuunguza umaskini katika shirika la wafadhili yaani NGO's iendelee katika nchi yetu bila kupakua sehemu nyingine yeyote katika Kenya. Na serikali ichuunguze maendeleo wanayofanya.

Pili, serekali ipatie watu wake chakula cha kutosha ili waziemie na njaa. Na pia ipatie wa Kenya loans za kishirika ama vikundi vya jamii.

Tatu, katiba ya Kenya iruhusu kifunguliwe na kuleeta viwanda ndogo ndogo karibu na watu kama vile Kenya meet commission, kahawa, chai, maziwa, pampa, sukari, saruuji na dhahabu, ufuta yaani simsim hapa Pokot maana hizo rasilmali itaweza kufanya vizuri hapa W. Pokot.

Ya nne, Katiba ya Kenya ipatie Wizara ya Kilimo pesa ya kutosha ya kuweza kusafirisha maofisa wa kilimo kufika kwa wakulima kwa haraka ili kuondoa umaskini lisifikie kwa watu kwa urahisi.

Ya tano, Idara ya Utawala ibaadilishwe kuwa Polisi, yaani askari wa AP. Iwekwe katika wizara ya mambo ya nchi ya Home Affairs na askari wa utawala. Na pili, lingine promotion ya sub-location iinuliwe kuwa location na nafasi ya Chief, ya katikati itolewe ile nafasi ya sub-chief iwe Chief ya location. Ili utawala unaweze kuwa karibu na watu. Na, ofisi ya D.O. iondolewe, ya DC ilibaki, ya PC itolewe kwa maana DC yuko pale. Wizara ya vyama vya ushirika ipewe uwezo wa kupatiana loans kupitia Cooperative Bank na iweze kwenda katika vikundi vya ushirika vijijini. Wazee wa kokwo pooy, wawekwe katika ngazi ya Division pekee yake ya District Level yaani Tribunal Court. Na hawa wazee, wahasike na kezi ndogo ndogo ya kijamii na zile kezi kubwa kubwa ziende kwa magistrate's courts na wazee hawa wa kokwoo poy wasipewe nafasi ya kutosha watu fine, ili magistrate's courts pekee.

Na Police ambayo itachukuwa nafasi ya Provincial Administration iwekwa katika Division Level na wawe wakifanya kazi pamoja na wazee wa kokwoo pooy kwa zile kezi ambazo zinahusu kijamii, ili wazee hawa, wasianzishe rushwa. Usajili vya vyama vya ushirika kiangalie sana wakati wa kusajili vikundi kama vile makanisa, kuangaliwa kanisa zile zinaweza kulete vurugu katika jiji kuwe ni kanisa sawa, kama vya kuabudu sanamu.

Katiba ya sasa ihusishe serikali ihusike na kupanga uzazi upunguze umaskini na kusomesha watoto kwa elimu ya bure na serikali isipate gharama nyingi.

Nyingine, tuwe na serekali ya majimbo kuanzia Province na District level na tuwe na serikali kuu ili ugawanyaji ya pesa ya serekali uwe sawa kila mahali.

Ya mwisho, waakilishi wawe kutoka katika Division na yule atapita katika division hiyo ikawekwee katika county council kama nominated councilor na nominated councilors iondolewe, na yule atakaye kujaa kama mwakilishi akae katika kikao cha Council na yule atakayepata nafasi ya kupita awe MP wa kuwakilisha watu kutoka Bunge. Nominated MP iondolewa.

Hayo ndiyo maoni yangu.

Com. Lethome: Umesema kwamba koti za wazee kuwe na faini, koti za wazee zamani hapa kwenu, zilikuwa zinaitishwa faini? Na kama haiitishi faini, kazi yake ni nini?

Mwinjilisti Samuel: Koti zipewe uwezo za kupiga watu faini kule division. Kuna faini ambazo watapatia watu kazi ndogo ya kuweza kusaidia hiyo division kama kunjenga barabare, ama kufanya kazi ambazo zingesaidia community hiyo kupanguza tatizo la wafungwa.

Com. Lethome: Asante sana. Paul Ngiro.

Paul Ngiro: Majina yangu ni Paul Ngiro. Kwa maoni yangu ya kwanza ni kuhusu dini ama makanisa, kwani ziko nyingi sana. Hasa kama ni mia nane arobaini na tanu hivi. Kuna kanisa ya sanamu au human sacrifice. Kwa kisheria, liwe makanisa matatu au manne, halafu tupate kuabudu sawasawa.

Ya pili juu ya hospitali katika West Pokot, kwa maana watu wote wana hama hama hospitali ijengwe katika location na government, apewe dawa hapo katika hospitali, kwa maana kama Lelan tumepataa manufaa, na kama tungekuwa na hospitali, tungeendelea vizuri.

Ya tatu, ni kuhusu shule, tuko tu na ishirini na hakuna government Sponsor ndani yake. Nii NGO's pekee yake. Sasa sheria iangalie W.Pokot vizuri, tujengewe shule sababu watoto wao ni nomadics.

Yangu ni hayo tuu, kutoka Paul Ngiro.

Com. Lethome: Asante sana Paul. Tutajaribu kufanya balance, Chepksuukuut Limakeriis. Mama karibu. Nyoni mama. Ametoka ehh. Ywotokia Lotimo.

Ywotosia Lotimong: *Kainenyaan kee kuroy nyoni. Otungetan ngal chole tukutee. Nyopo tagh kuu ngala skuutali ompo wolo nyopo tagh kuu sapon poo chii. Ato mominyee riipot nyopo chii kutoh piich sakuut kule kuh kiwonyo piich ompo Kenya.*

Translator: Jina langu ni Ywotosia Lotimong. Nina maneno machache tuu. Ya kwanza ni kuhusu hospitali maana uhai wa mtu ni kitu cha kwanza. Kama hakuna ulinzi kwa uhai wa mtu, watu wote watamalizika Kenya.

Lotimong: *Nyopo odenya kuu kusoma. Kiluku piich megh ompo ngala kusoma, mokmiteeni nyee mali. Nyo kak mochecha elimu kluuku kule.*

Translator: Ya pili, ni kuhusu elimu. Watu wamekuwa maskini kwa sababu ya kusomesha watato. Tungetaka elimu iwe ya bure.

Lotimong: *Nyopo somok, kmoochoy ompo W.Pokot kuu nguutu piich mpake ngwaa. Angwan, ompo wuudun cho miiteni West Pokot.*

Com. Lethome: Boundaries anataka nini? na forest anataka nini?

Lotimong: *Kmokoy kungutu piich rotwee ngwa mpake ngwa ompo West Pokot. Ompo Foresti, omochan kriip raia. Akekul piich cho ripoy foresti.*

Translator: Anataka Wapokot waonyeshwe mipaka yao. Pia anataka foresti raia wenyewe wachunge.

Lotimong: Nyopo po muut kmokecha kalya ompo koreencha kempuurocha nyo karaam. Kmokecha kotini nyo ngorokecha le raia. Soro nyo wou.

Translator: *Tunataka amani West Pokot tukae vizuri na pia tunataka koti hapa kwa ajili ya raia. Asante sana.*

Com. Lethome: Haya asante sana. Francis Moin yuko.

Francis Moin: Omwoghan lenye ngalechuu pogh petoy mpaka Kisumu nko Lake Victoria akmenguut nyee piichini lo pkonoy poghe chete ono. Mjini kekonecha piich po Highlands kupkaa kwipu pogh koro neete tukwil. Ompo wolo poishegho poghechete mpaka Kisumu hat Misri. Kakmokecha piipo koroonete kuyong chuu idara nonii melo piipo Kisumu. Teno choni chiichan.

Translator: Ninasema tuu kidogo kama vile maneno ya forest, kwamba kuna maji inatoka hapa mbaka Lake Victoria na hao watu hawajui maji yenyewe inatoka wapi. Hivyo ninataka wenyewe hapa nyumbani wachakuliwe wasimamie maji yao badala ya watu wa Kisumu kusimamia. Asante sana.

Com. Lethome: (in audible) Charles Rumot

Charles Rumot: Kwa majina ninaitwa Charles Rumot. Ninaongea tuu kidogo kuhusu ugawaji wa raslimali ya serikali. Inatakikana igawanywe kulingana na vile serekali iko. Kwa hivyo kila mwanchi ya Kenya ajuwe vile raslimali ya Kenya iko.

Ya pili, ni kuhusu sheria za nje. Sheria iandikwe ambaya hakutakuweco mahali mtu ananyanyaswa vile kuna mtu ambaye anaweza kuipa ng'ombe moja ya mahindi na mwingine aipe pesa ya mahindi milioni kuni. Mtu wa milioni kumi anafungwa mwaka tatu na mtu wa ng'ombe moja anafungwa mwaka kumi.

Ya tatu, hapa nyumbani kuwe na sheria ambayo inatoka chini kuangalia civil suit halafu criminal cases iende kotini. Hiyo civil suit iwe ya kimila. Ni hayo tuu.

Com. Lethome: Asante sana, Joel Arimoi

Joel Arimoi: Natoa shukrani kwa Commissioners we tume wa katiba mpya kwa kuja hapa West Pokot. Niko na maoni machache. Ningetaka elimi liwe pure kwa sababu watu wingi hawawezi kusomesha watoto wao. Wanamalizia daraza la nane.

Upande wa hospitali, ningetaka Health Centre watupatie magari ya kupeleka wagonjwa mahospitalini ili gharama iwe ndogo.

Upande ya mkasa wa area, vijijini, tunataka katiba itambue na kuwalipa mshahara kidogo mkasa kwani anashukulika na mambo mengi vijijini.

Com. Githome: Mkaza ni kwa wazee au kina mama?

Joel: Wazee tu

Com. Lethome: Hamtaki kina mama

Joel: Hata tukiwachanganya, hakuna shida.

Joel: Basi, upande wa forest, iwe mikoni ya raia ili wachunge vizuri kwa sababu watu wa DC wanakata kata saa zingine.

Com. Lethome: Ungetakaje?

Joel: Watu wenyewe wachunge. Na upande wa chokora, serikali wajenge mahali wasomeshe hao watoto. Na upande wa mamlaka wa raisi, ningependa sheria wabadilishe wa aweze pia kustakiwa ya Rais.

Kuna kuhama hama pia kwa ajili ya ng'ombe, serikali wapinge. Walete KMC karibu ili wasipotese mali wanapoona ng'ombe yao karibu inaangamia.

Ni hayo tuu.

Com. Lethome: Asante mzee. Wilson Chumwoy. Kina mama kueni huru msiwe ndani ya gari bila kuchangia. Kuweni na maneno ya kuchangia. Msikuwe tu , observers. Haya endelea

Wilson Chemwoy: Niko na mawili kuhusu katiba hii. Kuna elimu kwa upande wa shule za upili. Sio wengi wamefika kidato cha nne. Ningependa serikali waangalia kikazi. Sababu si wao ndiyo wamekosa.

Ya pili, wamama wapatie uhuru, wa kuendelea maisha yao.

Com. Githome: Endelea.

Wilson Chemwoy: Ya tatu ni kuhusu natural resources. Tuko na chemchemi ya maji. Ningependa mambo ya forest iangalie.

Com. Lethome: Sasa nani angalie na kupitia kwa nani?

Wilson: Serikali kupitia kwa mwananchi. Kwa maneno ya natural resources, sisi wenye hatufaidiki wengine ndio wanafaidika nayo.

Com. Lethome: Sasa ungependekeza nini?

Wilson: Ningeonelea wakate sehemu katikati kama vile Waturkana wanafaidika na samaki hata pia vile wachaluo wanafaidika. Asante.

Com. Lethome: Asante sana, Philip Lomongin.

Philip Lomongin: Nashukuru commissioner kwa kufika hapa. Asante sana. Kitu cha kwanza ni kuwa tangulizi yake. Kenya ni nchi ya nani? Sisi ni watu wa Kenya na makabila ya Kenya yote yaandikwe katiba.

Sisi Wapokoti tumetosheka na military operations. Kazi ya military ni kuchunga mpaka wa nchi siyo kupiga raia wa nchi hii. Tunataka District County Council wasimamie maneno yao wawe independent na wasisumbuliwe na provincial administrations. Wapewe funds kwa sababu wilaya maskini kama ya Pokot hawawezi kupata vitu vya maendeleo. Katiba ipewe Council nguvu na budget ya one billion katika wilaya zote za county council. Ili tuweze kusomesha watoto wetu, kuchenga parapara.

Tunataka District Service Commission ya kuangalia mambo ya kasi hapa kwetu kwa sababu Wilaya ya Pokot hata mpishi anatoka wilaya ingine. Sasa kusomesha watoto itakuwaje kama hawaandikwi kazi? Kwa hivyo tunataka kazi zote za Wilaya Yetu liandikiwe District Service Commission.

Ya tatu ni kuondoa Provincial Administration kwani iliumbwa kusimamia Waafrica na wakolini. Sasa tumepata huru na hatuoni kazi yao haza.

Kwa judiciary (inaudible). Tungeta sheria ya Mwafrika iwe parallel na ya wazungu. Na kezi yote ya Wapokot zianganiwe na traditional courts. Kama vile mtu anatoa ng'ombe sita akipatia msichana mimba na kuchukuwa mtoto wake akiwa mkubwa.

Com. Lethome: Na akitaka kumuoa?

Wilson: Akitaka kumwoa, atalipa mahari ya kusikisana. Katika mila za Kenya zote ni mila za Kenya hata kama ni ya Wapokot au Waturkana. Hivyo hakuna haja kupiga marufuku mila zetu.

Com. Lethome: Na zile harmful? Kama FGM

Wilson: Hiyo iondolewe kupitia dini na elimu siyo kupiga marufuku hiyo ni kama kutupa. Kwa sababu tunafurahia mila zetu.

Kwa President awe ni graduate na masomo ya juu. Asikuwe MP wa constituency ndiyo aweze kuangalia nchi yote. Awe ni mtu ameo na anaishi na jamii yake. Awe na two terms. Saidi ya hiyo asisimamie uchaguzi wowote wakati yuko kwa kati kwa sababu atatumia rasimali yote kuharibu. Chief Justice au Speaker wa National Assembly ashikilie kiti cha presidency wakati wa uchaguzi.

Kila mtu aliyezaliwa Kenya awe citizen wote awe kijana au msichana. Kwa sababu saa hizi yule mtoto kijana anaruhusiwa kuwa Kenya citizen na yule msichana haruhusiwi.

Tuwe na ID, passport and kitabu kidogo cha katiba ili mtu ajuwe ni nchi gani mtu yuko na sheria gani linamongoza. Watu wa Kisumu wanakunywa maji bila kujua maji inatoka wapi. Hivyo wananchi wenyewe wafaidike.

Corruption katika Kenya ni wasi na inakupalika. Kitu cha ajabu kweli.

Ya pili kwa sasa serekali inategemea tu kodi kutoka kwa national scheme. Asili mia sitini ya Wakenya ni masikini na viongozi wa Kenya wamenona sana Bw. Commissioner hata kusimama kwa kiti hawezi mpaka wajue kiti yenye iko gurudumu ya kufuta. Tungetaka serikali wachuwe ya kuwa ni sisi tuliwachagua. Hivyo budget itolewe ya kusimamia maneno haya. Mbeleni tulikuwa na AFC ambayo ilitusaidia watu wa Lelan tukabadilisha maisha lakini kutoka mwaka 1979, hatujaona kitu kama hicho.

Tungetaka AFC, FMR na loans yote irudishe na kuwekwe katika budget. Mkulima kwa miaka tano maneno yake hapana endelea wa. Wanaletewa Factory ambaye hata haina primary products.

Civil servants ambao wanalipwa mshahara, walipwe nono nono ili wasifanye biashara. Wasifanye kazi hiyo ya biashara maana watakosa kuwa mfanyi kazi wa serikali. Tunataka Human Rights Commission mpya ya kusitaki serikali au ofisa yeyote ambaye amefunja haki za mwana damu nchi hii.

Tunataka Land commission tofauti kutoka na koti zingine za Kenya. Mshahara wa wabunge utengenezwe na hii katiba uwe elfu mia moja.. Kubadilisha katiba iletwe kwa referendum. Na mshahara wa Raisi uwe Kshs.200,000-, councillor – Kshs.30,000- to 50,000-.

Land control hapa kwa Wapokot wachunguze mambo yao wenyewe kama vile title deeds zao, zipatikane hapa siyo Nairobi tu. Bw. Commissioner ni hayo tuu.

Com. Lethome: Umesema Rais lazima awe amera, lakini kuna watu wengine kama Catholic hawafungi ndoa. Ama Rais awe ni mwanamke. Hawa tutawafanyaje?

Wilson: Yule Rais ambaye hana family hajui chungu wa mwana. Kwa hivyo awe ni mtu ako na family hata kama ni Bishop.

Com. Lethome: Asante sana. Petro Akwangaluk.

Petro: Ninashukuru Commissioner leo kuja kusikia maoni yetu. Kwa muda sisi wakenya tumenyanyaswa hata tukienda kwa biashara. Tumepata shida nyingi sana kwa sababu ya Stock Theft. Hakuna kazi ambayo wanafanya. Wanahangaisha watu bure na kuwachukulia pesa.

Com Lethome: Sasa unataka wezi wa ng'ombe wahusikiwe na nani?

Petro: Wananchi wanaweza kuwashika. Na lingine ni kuhusu Assistant Chief, watolewe. Mkenya awe na uhuru wa kuuza vitu vyake kila mahali. Mtu awe na uhuru kuabudu Mungu wake.

Com: What about devil worship?

Petro: Hawezi kuabudiwa. Mungu tu ndiye aabudiwe.

Com. Lethome: Nelson Nguria, yuko? Karibu Nelson

Nelson Nguria: Basi kwa majina naitwa Nelson Nguria. Nashukuru sana kwa nafasi hii. Nina mambo machache tu ya kupendekeza kwenu Commissioner. Moja inahusu matibabu. Nengependa matibabu iwe bure kwa Wakenya. Halafu baada ya hapo, Private Clinics au hospitals should be abolished kwa sababu tumeona ya kwamba sisi kama Wapokot tumenyanyaswa sana. Tunanunua dawa kwa pesa nyingi sana kama Kshs.30- kwa tembe moja hivi, hivyo tunataka iondolewe kabisa.

Ya pili, ninaona kwa mtu ambaye anadunga miimba mtoto msichana apatiwe punishment ya Kshs.50,000- ili Wapokot wasome vizuri sana na kujenga nchi yao.

Ya tatu. Watu wa kupenda hongo washtakiwe ili ufisadi utupiliwe mbali. Serikali isaidie wamama wafanya biashara kidogo dogo ya kujinufaisha. Wapate elimu sio kuwachia wanaume tu pekee yao kufanya kazi. Wamama bia wapewe ruhusa ya kumiliki mali kama wazee pia na kupewa loan.

Com. Lethome: Wamama wamelalamika ya kwamba mambo ya shule ya watoto wameachiwa wazee peke yake.

Nelson: Ni kweli wamewachia. Mtu ashike jukumu yake ya kuchunga boma. Tunataka serikali kusaidia Pokot kujenga slaughter houses ili wauze nyama mahali inaweza patikana. Na market ya kuuza mahindi yao. Councillor awe mtu amehitimu Form IV with a mean grade of C+. Tunaongozwa na watu hawajui nothing, no vision no nothing. Asante ni hayo tuu. (laughter)

Com. Lethome: Asante sana ndugu Nelson, hebu tusikie sauti ya wamama sasa. Martha Mwok. Karibu

Martha Mwok: *Soro nyo wou nyoman, ompo kainotuut ko chan kekurenanun Martha Mwok. Nga nyona ompo yee ompo acha ngala yootun, kmitecha kemwoghey nyoman lo, angarakechane masomo monuung kungetunegho kopo tagh mpaka daraza la nane.*

Translator: Asante sana sana. Kwa jina ninaitwa Martha Mwok. Hivyo kwa sasa hivi tunaomba kwa ajili ya wamama watusomeshee watato kutoka daraza la kwanza hadi la nane.

Martha: *Ompo wolo kik nukishecha nyoman ompo yotuun kekepusweecha yotuun ompun nyoman. Lendoy pat wiyonyi nko munungee kuu kepusinyi msigo nay po monuung. Na anaende kwa nyumba hiyo ingine.*

Translator: Kwa sababu mzigo huu wa kusomesha watoto umekuwa mzito sana kwa sisi wamama kwa sababu wazee wametuachia peke yetu. Wanasema tu kaa na watoto wako na anaenda kwa nyumba ile nyingine.

Com. Lethome: Nyumba gani nyingine?

Martha: Ya mwanamke huyo mwingine, wameo tatu hadi nne.

Com. Sasa ungetaka sheria iseme nini kwa huyu mzee.

Martha: Wazee wasioe wake wengi ikiwezekana hivyo.

Com. Sheria ya Pokot inasema nini kuhusu haya? Mzee moja mwanamke moja?

Martha: *ompo wakati neete mokumukonye kwiip chii koor cho chang.*

Translator: Hati kwa wakati huu haiwezekani kuoia wanawake wengi.

Martha Mwok: *Nyopo odeny, kmoreecha kirwokoot ketaap lain klee ataye k'kuloy Kansellen, ompo wolo kiku nyanyasanecha yootun nyoman. Ompo wolo lenye ato kmungh chii ompo kau aiyipchinyi ngale kuu, mo iwuunyinye lawel.*

Translator: Ya pili, tunataka Chief achukuliwe na watu wakipanga kura kwa sababu wametunyanyaza sana wamama. Yaani kama mtu akipigwa, ukipelekea yeye hiyo kesi anagawia sa.

Com. Mtu akipiga mtu achukuliwe hatua gani?

Martha: Mtu akipiga mama afungwe. (laughter)

Com. Lethome: Endelea mama.

Martha: *Nyopo somok, kmokecha le vikundi no yotuun, kekul yoo akonga nyo yipkechaa ngale choo ompo wolo kikuwerecha ngala nyoman, moke lumecha nyee ngale chino pkonoy wono toka wono.*

Translator: Ya tatu ni tunataka vikundi vya wamama achaguliwe yule atatuletea mambo ya kutoka Bunge au sehemu za juu kwa sababu wazee hawawezi kutuambia haya.

Com. Lethome: Tuendele.

Martha: Asante sana sina mengi.

Com. Lethome: Tumesikia hapa kwamba wasichana hawagawii mali ni wazee tu ndiyo wanagawiwa. Na title deed lko kwa jina la mzee pekee yake. Sijui uko na maoni gani?

Martha: *Kmorecha ompo atani kechoghchini monuung chole tiipin tuku kwa aketo title deeds kunyoru chii ato ko par anda nee, ompo wolo miteni monungoo cho kikeiyichuu keston a mokunonoy nyee chi.*

Translator: Amesema kwamba watoto wote wasichana wagawie mali kama wavulana pia, kila mtu apate. Kwa sababu kuna wasichana wengine hawajaolewa hivyo wagawie mali pia.

Martha: *Kmokecha ompo kau kluku para yo nko papo ato mowogh papo kwalta paranay. Mchini kluku number akongo nko yotuun.*

Translator: Title deed iandikwe majina ya baba na mama ndiyo baba asiweze kuuza peke yake.

Com. Lethome: Haya asante sana mama. Jacob Kimeli yuko? Haya endelea James.

James Lokoreet: Mimi kwa majiina naitwa James Lokoreet, nasema ni asante. Kwanza ningetaka kusema maneno machache, ningependelea mali ya kirauni tuweke kando na Chief pekee yake afae uniform. Halafu Assistant Chief afutwee. Mzee wa mtaa achaguliwe na alipwe mshahara.

Ya pili, mnasikia kule Nairobi kuna wezi hata kila mahali. Na wakati wakipatikana na wananchi wapige ripoti na polisi wanakawia, na tunajua ya kwamba wakati askari alipooandikwa, alisema atauwawa mtuu ama yeye mwenyewe atauwaua. Wanakuja kushiika raia ya kwamba onyesheni huyo mtu na sisi kama waraia hakuna kitu cha kushikia mtu na wizi. Tunataka

askari wawe ni watu wa kusaidia wananchi.

Ya tatu, mambo ya Commissioners ambao wako kule Nairobi, sio President mwenyewe ambao anachagua, ni elimu ya mtu ambao amepita awe Commissioner. Kama ni wa Lands, Forest ama nini. Mtu ako na hati yake kuonyesha kwamba amesomea hii elimu. President anachagua hata kama hakuna elimu.

Co. Lethome: Sasa wachaguliwe na nani, commissioners?.

Lokoreet: Achakuliwe na makartasi yake vile amepita.

Co. Lethome: Nani ataangalia hizo karatasi.

Lokoreet: Kwa Wizaraa ambayo anataka.

James Lokoreet: Halafu mshahara ya Councillors. Isije ikakuja kutusumbua hapa. Kuna wamama wanaweka vitu yao kwa soko, na wanaitisha kitu kidogo. Tunataka Concillors walipwe kule Nairobi kama Bunge. Ikiwa ako na bibi nne, lazima ananyonya moja.

James: Eeh? Hapana cheka hii ni maoni yangu. Halafu nyingine. President awe chini ya sheria na sheria iwe juu. Kwa sababu mtu wa sheria akichaguliwa na President na mtoto wa President akikosa, anaenda kwa President na kumwambia, Bwana, tupa hiyo kesi. (Judge siyo mtuu wa sheria).

Com. Lethome: Haya endelea.

James: Jambo lingine kama pesa ikikwisha kama ya mshara wote katika district, sisi si ndio tunasimamia, ni ma-councillors na MP, na wazee ambao wamechaguliwa na wananchi ndio wanasimamia hiyo pesa. Kama ni ya barabara iende kwa barabara, isije ikapotea katika ofisi ya DC. Halafu ingine mimi naongea juu ya mashamba ambayo iko pale Kitale. Hakika sisi watoto na kuna babu yetu ambaye alikuwa anaishi, na kulingana na agreement ambayo alifanywa na wazungu, hiyo mashamba ni kuonyesha, na kama mtu akikodesha shamba la mtu, ni analima baadaye anaenda, na tunajua baada ya ya kwenda kuna wengine walikuja kunyakua hio mashamba.

Com. Lethome: Sasa unataka nini?

James: Tunataka hio shamba irudi na tunasikia somo kuna watu squatters, na katika dunia hii, Mungu hakufanya wengine kuwa squatters. Kuna mahali alikuwa anatoka na ni lazima mtu arudi kwake mahali alikuwa anatoka na shamba irudishwe kwa mwenyewe.

Com. Lethome: Sasa hio mashamba ya trans-Nzoia, wenyewe ni kina nani?

James: Ni sisi Pokot.

Com. Lethome: Kwa hivyo irudi kwa Wapokot.

James: Irudi kwa Pokot, ni hayo tu.

Com. Lethome: Asante sana Bwana James. Tupate sasa Richard Arusho, yuko? Ni Bwana Councillor, karibu,ambia wazee wasiongee tafadhali unajua tutapeleka tape Nairobi na makelele ndani yake.

Cllr. Richard: Majina yangu kamili ni Richard Arushwa. Kwanza na shukuru commissioner kwa kufika hapa kusikiza maoni yetu.

Maoni yangu ya kwanza, hii Katiba mpya tuwe na Bunge mbili, Upper House na Lower House, na tuwe na Prime Minister, na President ambaye atakuwa ceremonial President. Kuhusu county council, councillors. County council imesimamiwa na minister, na kuna officers ambao wanapewa cheo kuliko hata councillors ambaye wamechaguliwa ni wananchi. Kwa hivyo huo uwezo ya minister uwe wakisimamia peke yao, na hawa officers wawe manager. Sio officers wa serikali kama clerks. Wawe tu managers ambaye wanaandikwa na councillors ama county council.

Raslimali ambayo iko West Pokot ama pahali pengine popote kama Coast, minerals zozote tusihudimie mbali mtu ambaye anaitwa commissioner of minerals sasa. Hiyo tunaona ama kazi sababu anatawala ili kazi iko West Pokot ingine ama pahali pengine kama vitu kama minerals cost ama wanapatiana vitu huko pengine mtu yule anaweza. Kwa hivyo hii uwezo ya raslimali ipatiwe county council ya area. Pia commissioners wetu ambaye wanaendelea sa hii waandike hii Katiba mpaka wamalize. Ndio tuwe na Katiba nzuri mpya ambayo inatupeleka kwa uchaguzi.

Commissioners, sisi ambao tunaishi kwa hii mila ambayo tuko saa hii, hii milima kuna chemichemi zote za maji, na hizi chemi chemi zote za maji, tunalazimishwa kuzilinda bila kupatiwa mali yoyote na serikali. Kwa hivyo tungependa hii chemichemi, ya maji tupatiwe affirmative action kama kusomesha watoto wetu, halafu sisi tupate wale watu wa foresters ambao wanatoka hapa. Hii maji inamwagika Lake Victoria, Lake Turkana na inafaidi hawa, kwa hivyo sisi tungetaka tukatiwe kama deduction kusomesha watoto kwa secondary, halafu sisi tupate elimu.

Pia ya mwisho ningependa serikali itupatie Kenya Meat Commission kati yetu na Turkana ili tuuze ngombe yetu sababu sisi ni wafugaji wa ngombe. Kwa hivyo tupate kitu kama Kenya Meat Commission. Commissioners nafikiri mimi nimefika mwisho, nasema asante sana.

Com. Lethome: Tafadhali Bwana Councillor ya kwanza, nataka unigusie habari ya elimu ya ma-councillor unapendekeza wawe na kiwango gani cha elimu, hio moja. Ya pili, ningependa uzungumzie habari ya mshahara ya councillors, unasema nini? Na ya tatu ningependa uzungumzie habari ya nominated councillors, utasema nini? Maswali matatu hayo tueleze.

Cllr. Richard: Commissioners, ni kweli kwamba tukitaka kwamba wilaya iendelee vizuri, na tupate mambo yote sawasawa, kiwango cha elimu iwe 'O' level kiwango cha secondary.

Com. Lethome: Grade gani?

Cllr. Richard: Kwanzia grade ya B na kuendelea. Halafu umeuliza mimi habari ya?

Com. Lethome: Mshahara wa councillors.

Cllr. Richard: Mishahara ya councillors. Unajua councillor ni mtu ambaye yuko karibu na mwananchi wa kawaida, na yeye ndio kila siki shida zote za area hio zinaenda kwake. Kwa hivyo kwa maoni yangu ningependa councillor apewe 50,000/= ama zaidi.

Com. Lethome: Okay, itoke wapi mshahara? Central Government.

Cllr. Richard: Mshahara hio itoke kwa Central Government kama ile ya wajumbe. Swali la tatu, ilikuwa?

Com. Lethome: Nominated councillors.

Cllr. Richard: Nominated councillors wachaguliwe kulingana na mahitaji, kama pengine ni kuwakilisha kina wamama, ama kuwakilisha vijana, ama kuwakilisha walemavu. Tuwe na hio uchaguzi wa nominated councillors lakini, kulingana na watu ambao wanawakilishwa.

Com. Lethome: Yaani special interested group?

Cllr. Richard: Special interested group.

Com. Lethome: Asante sana Bwana Councillor, jilandikishe. Sasa tumpate mama, mama tunaye sasa naye atazungumza huyu Kucheruto ni mama.

Audience: Ndio

Com. Lethome: Haya mama, Kocheruto, majina yako?

Ko-cheruto: *Kainotuut ko chaan kuu, Koo Cheruto*

Translator: Anaitwa Kocheruto Katwa.

Com. Lethome: Endelea.

Kocheruto: *Tanga tagh*

Translator: Ile kitu angesema,

Kocheruto: *kugh nyo komwoghan kuu*

Translator: Ni kuhusu hospitali kama ya district Kapenguria.

Kocheruto: *Kleenyee ngala ospitaliin*

Translator: Angependa madawa yawe bure.

Kocheruto: *Kmookeecha sakuut chopo kule*

Translator: Kwa sababu hata hao madaktari wameajiriwa na serikali na wanapata mshahara ya serikali.

Kocheruto: *Ompo wolo liponoy sooch Chepsakutiis chooni*

Translator: kwa sababu hata za huko pia kuna watu wokusukumwa hata kwa line, na wengine wanachukuliwa kwa hivyo hapo madaktari pia waangalie.

Kocheruto: *ompowolo miiteni piich cho kuyuumtoy ompo tarataa "line" nyoo mchiini chepsakutiis kuros*

Translator: Basi hayo ni maoni yake.

Com. Lethome: Mama unasemaje mambo ya wasichana kugawiwa mali na shamba, unasema nini?

Kocheruto: *Imwoghenyii loo nee tiipin keto tukuun nyaa?*

Translator: Habari ya masomo pia

Kocheruto: ompo ngala masomo nyopo kulee

Translator: Kwa hivyo wasichana ni vizuri wapewe mali sawa, na vijana pia.

Com. Lethome: Haya, habari ya masomo.

Kocheruto: *Ompo ngala masomo*

Translator: Yote wanatakikana kupata masomo, wasichana kwa wavulana wote, wasichana wawe na masomo sawa.

Com. Lethome: Kuna matatizo yoyote kuhusu mambo ya kusoma, kuna wengine wanasema wanataka, masomo ya bure. Yeye anataka ninni?

Kocheruto: *Imochenyii nee nyaa weyoo ompo masomo?*

Translator: Anasema pia masomo yawe ya bure kutoka daraza la kwanza, nursery mpaka Std 8. Halafu kuelekea Form 1, wazazi waangalie hapo.

Vicent Chimoruk: Haya asante sana. Kwa leo, hii ni wakati ya katiba. Tunashukuru sana kwa maneno ya katiba yenu kuhusu... (interjection)

Com. Bishop Kariuki: Usiseme katiba yenu, katiba yetu.

Vincent Chimoruk: Katiba yetu (Laughter) nimekosea.

Com. Bishop Kariuki: (Not clear).

Vincent Chimoruk: Kuhusu binadamu. Katika idara ya serikali yote ya Kenya lazima zipunguzwe ziwe chache. Kwa sababu zikipunguzwa iwe machache na bado watu wanaongezeka watu watakuwa wadogo kama idara zikirekebishwa ziwe chache.

Com. Bishop Kariuki: Ndio. Endelea.

Vincent Chimoruk: Owoy, tanga tagh.

Translator: Kuhusu serekali.

Vincent Chimoruk: Wale wanashika bunduki...

Vincent Chimoruk: Lazima waandikwe hata mtu yule hajasoma.

Com. Bishop Kariuki: Okay, endelea

Vincent Chimoruk: Kwa sababu kazi yake ni kushika watu. Kwa sababu watu ni... kuna wengine hawajasoma na lazima wasaidie kuandika hawa. Wale wamesoma, kila mtu na idara yake, kulingana na masomo yake.

Com. Bishop Kariuki: Ndio ingine.

Vincent Chimoruk: Yale watu wanasema walimu waandikwe mpaka kutoka nursery mpaka darasa la saba vile nane na mishahara ya serikali ilipwe.

Com. Bishop Kariuki: Kuna lingine?

Vincent Chimoruk: Malipo ya shule kuanzia 1 mpaka 8 hakuna kulipa pesa (Laughter). Hata watu ya form 4 pia, lazima waangaliwe hata wale wengine hawana vitu. Lazima isaidiwe.

Com. Bishop Kariuki: Masomo ya bure. Haya endelea.

Vincent Chimoruk: Kwa sababu kuna wengine hawana mali.

Com. Bishop Kariuki: Hiyo imeingia. Inginge.

Vincent Chimoruk: Lazima nafikiri nimetosheka.

Com. Bishop Kariuki: Haya tunyamazeni tusikize. Limokar Ng'uriandua ama Gurianua. Karibu mzee.

Interjection: (Not clear)

Translator: Nashukuru kwa nyinyi ambao mmekuja upande huu kwa ajili ya mambo ya katiba.

Limokar Gurianua: Soro nyo wou ompo akwaa choo ka pkanakwaa aswanetee.

Translator: Sasa anapendekeza ya kwamba kuwepo na security team ambayo inawekwa mpakani ya Karamonong huko chini mpaka kwa kila kabila.

Limokar Gurianua: Turkana

Translator: Turkana

Limokar Gurianua: Marakwet

Translator: Marakwet, Karamojong huko.

Limokar Gurianua: Mchiino kumii teeni ripoto koro Trkana, Marweet nko Karamojong,

Translator: Ya pili ni kuhusu maji ambayo tuko nayo upande huu.

Limokar Gurianua: Nyopo odeny, kuu ngala pogh cho momiiteni nyee koroo neete.

Translator: Tunataka wale watu ambao wananufaika sana kwa hii maji ambayo yanatoka katika milima hii kuelekea upande wa Lake Victoria, watupaties quota yetu ili sisi tupate kupanda miti area hii ya chemichemi.

Limokar Gurianua: Mchiini kee koneecha owezyo kekatkatachaa keet, to kenyoruno chaa chemchemii nyo tukwil.

Translator: Ni kuhusu wale watu wa kudunga ng'ombe, wa veterinary, Veterinary officers, ya kwamba siku hizi ni wachache sana na anapendekeza kwamba ni vizuri watu wenyewe waelimishwe juu ya kudunga ng'ombe wao na hata wanyama wao ili wao wenyewe waende kufanya kazi hiyo bila hata kuwasiliana na Officer. Pengine ma-officers siku hizi ni wachache sana.

Com. Bishop Kariuki: Hebu muambie kwamba yale ameyazungumza yamerudiwa, kuna time kidogo sana. Pilot ametuambia mvua ikinyesha ndege itakuwa na shida kuruka. Kwa hivyo tunataka tuna dakika chache sana za kutoka hapa. Kwa hivyo mtu asirudie yale ambayo yamezungumziwa, tafadhali.

Translator: Tunataka pia kuhusu forest yetu iwe juu yetu na sisi tuwe watu wakuangalie mambo ya forest hiyo na miti yoyote ili mtu isitoke mbali na kuja kuharibu na kukata.

Limokar Gurianua: *Kmokeecha wuudun neecha kmiiteni moriichaa nko parakuu chaa ata menguun nyuu chii ompo wolo low kunyar akuutoor keet.*

Translator: Kuhusu hata mambo ya sitima kama hii ambayo inatoka kwetu hapa, tunataka pesa yake ambayo inatoka ndani itumike pia katika area kutusaidia sisi. (Kipokot).

Limokar Gurianua: *Ompo ngala stimaa, nyopo Kositoy, mchiini kenyorunoo chaa ropyeeni kungarakeecha tikwil lenyee tekaataaa projectinoo Pokot.*

Translator: Asante.

Com. Luthome: Asante pia wewe. William Lokoloi, William? Hayuko, Geoffrey Lokido.

Geoffrey Lokido: Asante sana Commissioner kwani nimepata nafasi special kweli. Mimi kwa majina naitwa Geoffrey Lokudo na nilikuwa nafanya kama C.C.C. yaani Kamati ya kuangalia mambo ya Katiba. Katiba sehemu ya wakilishi bungeni

hapa Sigor. Ningependa niseme machache tu kwa sababu mengi yamesemwa, sitarudia. Lakini kuna jambo moja hapa inanisumbua sana na ningependa nirudie, samahani.

Com. Luthome: Sawa.

Goefrey Lokido: Lokudo. Hili swala ni swala la mishahara ya wajumbe, mishahara ya M.P.s. M.Ps tumewachagua ili waende kutuwakilisha kwa mambo mengi sana. Na wanafika kule, kazi yao inatushangaza. Hivi majuzi walimu walikuwa wakiomba nyongeza ya mishahara na hakuna kitu ambacho kimetokea kujaribu kuwasaidia hao na wafanyi kazi wengine wa serikali.

Tunasikitika sana kusikia sasa wajumbe wako na mpango sasa wa kujiongezea mishahara. Hali kadhalika, wafanyi kazi wengine wa serikali wako na Mishahara ya chini sana. Kwa hivyo, napendekeza kuwa tuwe na tume huru, independent commission, ya kuchunguza mishahara ya wajumbe. Hii tume iwekwe katika katiba, entrenched in the constitution na isiingiliwe na serikali kwa njia yoyote. Kwa hivyo iwekwe tutafute tume ile iko, independent itaweza kuchunguza mambo ya mishahara ya wajumbe. Kwa sasa, commission mbali mbali haziko na uhuru.

Jambo la pili nikuhusu mambo ya civic education, na tume ya kuangalia mambo ya katiba. Ningependa kukuarifu Bwana Commissioner kwamba, vile tulivyo sasa hawa watu wengi sana hawana habari kuhusu mambo ya katiba. Ni wachache tu, tumeweza kuwafikia na pengine hata wengine wanashangaa hii mambo ya katiba ni yakuingilia serikali au ni mambo gani hii.

Kwa hivyo, tungependelea mambo ya civic education, kufundisha wananchi iendele. Vilevile, mambo ya pesa, kufunza wananchi, hawajapata hiyo taratibu vizuri sana. Ningependa kusema katika nafasi hii kwamba sisi wale kamati wa sehemu ya uwakilishi bungeni tulikuwa tunalipwa shilingi mia tona kwa kila nafasi ya mkutano.

Na pesa ya kufundisha watu hatukuweza kupata. Tuliweza kuapply kwa sponsors kama vil DAF, CJPC na tuliweza kupata msaada. Ni juzi tu, last week minute ndio tuliweza tu kupata msaada kidogo hii ya mobilization embayo tuliweza kugawa pesa kidogo ikafika tena, na nilikuwa na mkutano ya vijana hapa, youth forum bata hapo kuna makaratasi. Na watu wanafikiri tuko na pesa kwa hivyo tungependa tuseme tunataka tuwe na ile transparency, uwazi ya pesa, na tujuwe pesa ngapi serikali imependa kwa kufundisha wananchi na hii pesa ijulikane kuanzia juu mpaka chini.

Lakini ninasema ninapendekeza kwamba iwapo pesa itapatikana ya kufundisha wananchi, na ipitie mashiriki ya makanisa kama vile CJPC na DAF na mengine, Pia CKRC yaani tume ya kurekebisha mambo ya katiba. Kuna trends of government mimi najua wameongea sitaki nirudie.

Ufisadi, hii ni tisho kubwa sana katika maisha yetu hapa Kenya, ni janga kama swali la ukimwi. Tungependelea kuwa, serikali

itenge pesa kiasi fulani for creating awareness, among all sorts of lives in Kenya. Tungependa kuwa na incentive fulani ya kuokoa nchi yetu, ili tuweze kufundisha kuanzia na viongozi wa kuu wa serikali tufundishe wanjumbe, tuje tufunze civil servants na tufundishe wananchi pia. Kwa sababu hakuna mtu ambaye ako safe, kila mtu ni mshirika wa corruption.

Jambo karibu la mwisho, ni mambo ya ukulima. Unajua hii ni sector moja ambayo inatupa pesa katika nchi yetu na tumeona sehemu nyingi zimezorota kama vile kahawa, nafaka. Napendekeza kuwa wakulima wenyewe wachanguwe wakurugenzi ambao wanasimamia almasi kama vile nafaka, maua, pyrethrum, kahawa na chai. Haya, katiba iwape uwezo wa kusimamia shughuli zote hasa kutafuta soko hizi mimea. Tunasikia kuwa kuna Pyrethrum Board of Kenya, National Cereal Produce Board, na hawa watu wanashikilia tu, National hatuwaoni, hatuwapati. Kwa hivyo ninapendekeza tuwe na pengine wakurugenzi kama vile sehemu wanaokuja hii mimea. Na majina kama Kenya Pyrethrum Board ibadilishwe kama Lelan Pyrethrum Board of Kenya, Molo Pyrethrum Board of Kenya na kadhalika.

Hii ni ya mwisho, Roads Boards of Kenya, naona serikali ilifanya mpango ya kuwa na ile Board ya barabara. Tunapendelea sana tuanzishe kamati katika wilaya ya kuangalia mambo ya mabarabara. Na tunataka wale watu wanatumia mabarabara, wana magari zao ndio watu watakao chaguliwa katika ile Board. Sio kuchanguliwa mtu ambaye hata hajui shida ya barabara, mpaka hapa, asante sana Commissioner.

Julius Topila: Asante Bwana Commissioners, kwa majina ni Julius Topila, ndiye mwenyekiti wa hii kanisa na member ya C.J.P.C. Najua tu wengi wameongea kuhusu yale yote yamesemwa na wakati umeenda, siwezi kurudia. Nitaanzia kwa kusema, nitaanzia kwa grass-lands, hiki kitu ipigwe marufuku katika katiba hii mpya kwa sababu kuna hii nchi ambayo iko na raslimali nyingi na ikiwa chini ya serikali, wale wahusika watapata hasara. Kwa hivyo, ningependekeza kwamba, grass-lands iwe tu ichorewe wenye wanahusika.

Basi ya pili, kuhusu Title Deed ya mashamba. Hii itolewe kortini na ipelekwe mahali shamba yenyewe iko kuwatoa watu huko, na hii kesi itaendelea vizuri kwa sababu wakati watu watakapoenda kortini watawacha shamba huko na wanaenda mkono mtupu. Kw hivyo hii kitu iwe kwenye shamba.

Basi kuhusu ofisi ya chief. Hii ofisi ipigwe marufuku, badala yake wachague wazee wawe na kundi ambayo inaitwa Pokot na pili ikuwe Pokot Two. Hii itasaidia sana kusuluhisha yale matatizo ya raia. Haya, kuhusu kilimo, wakati AFC ilipopotea, basi nchi ikakuwa maskini. Ningependekeza kwamba, word ile Agricultural Finance Committee itumiwe na ilete pesa, watengenze pesa nyingi sana ili wapeane mkopo kwa wakulima kusudi nchi hii inuke na pia wale wa National Cereals Board, wafunguwe buying centers halafu iwe karibu na mkulima.

Kuhusu dawa, watu wamesema juu yake iwe issue kuhusu security. Pia hiyo iko na passport iwe karibu na ipeanwe kwa kila Mkenya ile ameweza kuwa na title deed ili ipatikane kuwa akitaka kusafiri kusiwe na matatizo. Mwisho, kwa sababu saa

imeenda, hiki kitabu cha katiba ikiwezekana iwe Mkenya awe na hii kitabu ili ajuwe kwamba anatawalwa kivipi. Bwana Commissioner asante.

Com. Luthome: Joshua Lokotodo. Halafu afatwe na atondosia chemotwa, yuko? Haya ndio atafata huyo mzee. Tufanye chap chap.

Translator: Nashukuru sana.

Joshua Lokotodo: *Soro nyo wou*

Translator: Anaitwa Joshua Lokotodo.

Joshua Lokotodo: *Kurenanuun Joshua Lokortodo*

Translator: Kile kitu kimeleta umaskini hapa ni elimu.

Joshua Lokotodo: *Kugh nyo susaanuun chiik kuu nyo keepu meghwondon koronu, kuu elimu*

Translator: Erea hii ya Pokot.

Joshua Lokotodo: *Koronuu po Pokot*

Translator: Wale, rika yake yote hawajapata mshahara hapa Kenya sasa, kwa maisha yake.

Joshua Lokotodo: *Piich chole kongoot yee chaan, monyoruu nyee ropyeenichuu po Kenya.*

Translator: Anataka masomo yawe ya bure.

Joshua Lokotodo: *Mochay masomo kuluku kule*

Translator: Kwa sababu wakati hawa wanaona mwanagaza ya kwamba hawasomeshi watoto, fees inawauwa sasa.

Joshua Lokotodo: *Ompo wolo otini kaksuwechaa lo kesomeshono monungee kutungeechaa ropyeeni skuul*

Translator: Lingine, Kuhusu raslimali za Pokot wote.

Joshua Lokotodo: *Tukuun chopo Pokot*

Translator: Tumeona watu wa kutoka Nairobi wanakuja tu na Senyenge yake anakuja kufence upande huu akiona kuna madini fulani fulani.

Com. Luthome: Kama ruby.

Translator: *Kaksuweecha loo pkonoy piich lenyee Nairobi kuwaak paat tukuu chaa ompo nee?*

Com. Luthome: (Not clear)

Translator: Tunataka sasa hivi vitu vyote viwe chini ya Wapokot wenyewe.

Joseph Lokotodo: *Kmokeecha tukuu chaa kumii teni moriichaa.*

Translator: Asante

Com. Luthome: *(soro nyo wou) (Laughter)*

Background Conversation: (Kipokot)

Atonetosa Chemotwo: *Soro weena Commissioner*

Translator: Asante sana Commissioner.

Translator: Sasa leo ndio tumejua maana ya katiba.

Atonetosa Chemotwo: Ko kinguuchaa nyuu yee maana katiba

Translator: Anataka mshahara yote ya wabunge pamoja na wafanyi kazi, wote we serikali kuwa sawa.

Atonetosa Chemotwo: *Koo omochan mshahara lowur chopo Kenya kukaar kegh nko chopo wabungen.*

Translator: Ya pili...

Atonetosa Chemotwo: *Nyopo odeny*

Translator: Tunataka mtu hata kwa mfano kwa Mpokot akiua mtu mmoja kuweko na sheria ya Pokot ambayo inaitwa Lapai ambayo wao wenyewe wanajua vile ya kusuluhisha na malipo yake.

Atonetosa Chemotwo: *Omochan ngala lapay ato tugh chii chii.*

Translator: Tunataka pia kama Wapokot usawa ya kuwa na chuo ya walimu kama colleges ya walimu au yoyote, kama vile Kenyatta alifungwa hapa, hatukuwa na faida yoyote ya kwake sasa. Ni vizuri tuwe na college yoyote ya walimu ama nyingine.

Atonetosa Chemotwo: *Kmokeecha colleges chopo waliimu, kulee otiino kikiraatnyuu Kenyatta Kapenguria, take karachaa kegh lee piich walak.*

Translator: ...ili tuwe sawa na watu wengine wote.

Atonetosa Chemotwo: *Atakekarachaa key lee piipo Kenya.*

Translator: Kuhusu chiefs.

Atonetosia Chemotwo: *Kleenye Kirwakoot*

Translator: Anatakikana kufuta yote kutoka chief mpaka D.C. pekee yake ndio anabaki na D.C. awe hapo tu hana nguvu yoyote, ni mtu tu wa kupeana report huko juu. (Laughter).

Atonetosia Chemotwo: *Mchiini kevuutan kungetunegho kikwokoot mpaka DC, ak luuku DC paat chii nyo totoy ngaal paat wono toka.*

Translator: Kutoka sub-location tunachagua mkasa, na hiyo ni kwa kura ya mlolongo, mpaka location pia achanguliwe ile ya mlolongo.

Atonetosia Chemotwo: *Kekuul mkazeen kungetuuno sub-location ompo kureen*

Translator: County Council sasa.

Atonetosia Chemotwo: *ompo ngala Country Council*

Translator: Anapendekeza Councillor kwa sababu uongozi unatoka kwa Mungu na hekima yote inatoka kwa Mungu na hekima yote inatoka kwa Mungu. Kwa hivyo mtu anaweza kuwa na hekima bila masomo. Kwa hivyo achaguliwe bora amemaliza darasa la saba kuendelea kwa wadiwani.

Atonetosia Chemotwo: *Mchiini kekuul chii kurupaategha akilinyii mendo ompo masomo, bora paat kikureel kopo muut nko odeny.*

Translator: Haya ni hayo tu... Uchaguzi; watu wachaguliwe na wawe wa area hiyo na wasitawale sasa sisi. Asante.

Com. Luthome: (Not clear) Jackson Chemel, Jackson? Asante, Jackson Chemel ameenda? Haya tupate sasa Kapelitero Lokito, Lokiko. Rapelitero Lokiko, ameenda? Kama ameenda wacha tu usimuite. Saa hizi, (laughter), Thomas Yaranyang. Karibu haraka haraka kijana. Halafu tuna huyu mwengine wanga Koropoi. Koropoi yuko?. Hakuna. Usiite ule hayuko. Usiite yule ambaye hayuko hapa.

Thomas Yaranyang: Kwa majina ni Thomas Yaranyang. Asante sana Bwana Commissioner. Ningependekeza ya kwamba ingawa yamesemwa na watu mimi narudi tena.

Com. Luthome: Haya.

Thomas Yaranyang: Kwamba masomo kuanzia nursery hadi kwenda mbele iwe free.

Com. Luthome: Ooh.

Thomas Yaranyang: Ya pili hospitali, pesa ya hospitali ipunguzwe kwa sababu unaweza kufa kwa sababu ya shilingi kumi,

ama ishirini, unapata kifo tu kama huna pesa. Sina mengi ya kusema, ni hayo tu.

Com. Luthome: Haya asante sana (claps). Sasa, nafikiria watu wa hii kanisa mafuta, wamemaliza wao? Kwa hivyo Eliya tuko na document yenu, Eliya nanangole. Hiyo tushapata yenu. Richard Lemangole, nafikiri ni hiyo hiyo church eh. Walikuwa na choir. Choir tutapata siku nyingine usijali. Haya, wacha tupate watu ambao wanazungumza. Tumpate Lematia kuchungura yuko? Haya karibu mzee.

Lematia K. : *Karibu poyoon.*

Translator: Tunashukuru sana.

Lematia K. : *Kak mwaghachaa lo soro.*

Translator: Anapendekeza vitu vyote, mali zetu zote ambazo district hii inatakikana kupata ziwe hapa na tupewe hapa.

Lematia K. : Kwanza

Translator: Anataka sasa mambo hii ya kutoa pesa kwa title deed ambayo umekuwa nayo ipigwe marufuku.

Com. Luthome: Kwa hivyo wapeane free?

Translator: Eeh, free na waside kwa sababu sasa wanasema kuna percentage fulani ambayo hata kama hakuwa na title deed utalipa. Iwe free kabisa.

Com. Luthome: Okay, hiyo tumemaliza.

Lematia K: Pande ya dawa...

Com. Luthome: Eeh.

Lematia K: ...Kabisa tumekwisha, wakati nilikuwa hospitali ya bure (interjection)

Com. Luthome: Sasa unataka nini hiyo hospitali?

Lematia K: Iwe ya bure kabisa kusaidia sisi (laughter). Hiyo sasa tumeeleza hiyo?

Com. Luthome: Hayo hiyo tumemaliza. Hospitali ni ya bure kabisa.

Lematia K: Haya, watoto pia wasome bure.

Com. Luthome: Haya, umepata hiyo.

Lematia K: Inaonekana ni chache tu ambayo...

Translator: Asante.

Com. Luthome: Asante sana mzee. Tumepata hiyo vizuri sana. William Korkon. Hayuko, msimuite muache tu hivyo hivyo. William Korkou hayuko. Tumepate sasa kama Chebet Lotong, huyu ni elder kutoka Kalontari. Yuko mzee, kuna Chebet Lotong? Ni mama.?

Background Interjection: (Not clear)

Com. Luthome: Basi hayuko. Mwache. Kama hakuna unawacha. Haya, tumpate, Samuel Kudo.. Kudosu ama Kadoso? Kodoso. Yuko? Kodoso hayuko eh. Usimuite, muache. Haya tumpate sasa Daniel Tirokwang. Hayuko, usimuite. Nani?

Background Interjection: Daniel

Com. Luthome: Haya ingia Daniel. Halafu kuna mtu anaitwa Joel Kitaduna, Joel? Hayuko, msimuite. Haya, tuendelea.

Daniel T: Haya luutuno nyuu Daniel.

Translator: Nashukuru.

Daniel T: soro

Com. Luthome: Jina, Daniel nani?

Daniel T: Daniel Tirokwang.

Com. Luthome: Haya endelea.

Daniel T: *Tanga tagh*

Translator: Anapendekeza college iwekwe katika wilaya hii ya Pokot.

Daniel T: *College ompo koroo Pokot*

Translator: Pia anapendekeza, mwalimu wa nursery school apate mshahara yake kutoka kwa idara hiyo ya elimu.

Daniel T: Mchiini mwaliimnyoondo Nasari (nursery) kunyoru mshahara ompo idara nyopo waliimuun

Translator: Pia kuweco na security kubwa kwa wanyama wetu, hasa sana upande wa ng'ombe.

Daniel T: Asante.

Luthome: Asante sana. Haya tupate Lemanyak Riwaruk, hayuko. Tupate Daniel, huyu ni elder kutoka Bulunye. Haya, Daniel. Omuk. (Whispers).

Daniel Omuk: Asante sana Bwana Commissioner. Nina maoni matatu hapa hivi. Kwa majina ni Daniel Omuk. Ya kwanza; ningependelea kuwa kwa upande wa kilimo, wakulima wanateseka sana kwa upande wa market ama vile kuuza mazao yao.

Kwa hivyo ningependekeza tuwe na market ambayo iko-ready kwa wakulima.

Halafu ya pili, kwa upande wa employment haswa wale wanaenda training colleges ama universities kwa hivyo iwe na employment ambayo ni guarantee. Kwa hivyo ninasema ni asante.

Com. Luthome: Okay, asante sana. Lomukule Mathayo, hayuko. Haya Lotwari Sammy. Sijui ni Lotwari. Sammy asante sana, karibu.

Sammy Lotwari: Bwana Commissioner, mengi yamesemwa lakini tungependa pengine kusema kwa ufupi.

Com. Luthome: Aanza kwa majina yako.

Sammy Lotwari: Majina yangu ni Lotwari Sammy. Nina mambo matatu nita-summarise tu kwa ufupi kwa sababu ya wakati vile ulivyosema. Kitu cha kwanza ni upande wa kilimo, ama agriculture kwa jumla. Unajua kwamba katika hii wilaya yetu kuna sehemu kame na katika hizi sehemu kame tunapata kuona kwamba serikali kwa njia zingine wanapata kusaidia wananchi wale ambao wanaishi mahali pale. Labda kuwapatia chakula ile ready-made. Kwa maoni yangu ningesema badala ya kuwapa chakula wale, mambo mengine yangefikiriwa zaidi haswa kama vile mambo ya irrigation ili wao pia wapate kufanya kazi kwa sababu hiyo inachungia ule uvivu.

Jambo lingine ningependa kupendekeza ni usawa wa mishahara. Nikijaribu kuangalia ama kutazama jinsi wafanyi kazi wa serikali wanavyolipwa sio sawa kwa sababu unapata kuona kwamba kuna mtu fulani yule ambaye anafanya kazi yake lakini malipo yake ni chine sana kiasi kwamba yeye amelazimika kutafuta juhudi zingine zile zinaweza kumfanya ili apate pengine kuishi vyema vile. Ningeweza pengine kutekeleza, kidogo, haswa walimu. Wao ujira wao ni ndogo kiasi kwamba wanalazimika pengine wafanye biashara upande ule mwingine, wajaribu mambo mengine, wao wapatiwe malipo kulingana na kazi yao ile wao wanafanya maanake wao wanafanya kazi nyingi.

Jambo la tatu, kuhusu sheria. Naona, nikijaribu kuangalia mambo ya mahakama, vile watu wanavyotekelezwa na serikali hii haitoshi kwa sababu watu wengine wanachukua nafasi ama fursa hiyo kunyanyasa wengine. Ikiwa pengine watu fulani kama watu Fulani wamegombana ama wamekosana kwa jambo fulani na wao waende kortini, kuna wengine wajuaji sana na wanatumia nafasi hiyo. Kwa hivyo ningependekeza ikiwa jambo limetokea mahali ama mahali fulani, wale watu wa mahali pale kukuwe na korti ile inaweza pengine kutoa namuzi na kusuluhisha mambo yale. Kwa sababu ya wakati, nasema asante.

Com. Luthome: Haya asante sana.

Sammy Lotwari: Haya mambo yangu mengi.

Com. Luthome: Mambo mengi iko wapi?

Sammy Lotwari: Hapa.

Com. Luthome: Haya tutasoma tupate sasa wamama. Muda mrefu hatujasikia sauti yao. Monica Lonyangoseng kutoka Chepkong'o halafu afuatwe na Jesaku Elita. Hao wamama wawili.

Sammy Lotwari: *Nko yootunee chonii nyaa?*

Translator: Anatoa maoni yake kuhusu waunguzi ya kwamba ni vizuri kuweko na training ya wamama wazee ambao wanaweza kufanya hiyo, kazi wakuweko karibu.

Com. Luthome: Mid-wife?

Sammy Lotwari: Mid-wife?

Translator: Eeh.

Com. Luthome: Okay

Sammy Lotwari: Eeh.

Com. Luthome: Endelea.

Monica L.: *Tanga tagh*

Translator: Kwa sababu ya mahospitali yako mbali mbali, ni vizuri ku-train wa

Walewako karibu ili iwasaidie wakiwa karibu, wakiwa...

Monica L.: *Ompo wolo lowoch ospitaliin mchiini kumiiteni yootuno cho miiteni ato lekuut*

Translator: Ni hayo tu, asante sana.

Com. Luthome: Amesema mambo mengi. Mama mwingine anaitwa aje Chesakuu Eliza, ni wewe? Anza na jina lako.

Jesalem Eleso: *Mwagha kayuuneenguu*

Translator: Anaitwa Jesalem Eleso.

Jesalem Eleso: *Kureenanuun Jesalam Eleso*

Translator: Yeye anaonelea ya kwamba watoto ambao wamesoma mpaka form 4 wapate kazi, waajiriwe.

Translator: Kwamba, watoto ambao wamesoma mpaka form four wapate kazi, waajiriwe.

Jesalem Eleso: *Kmokechaa monungee cha kunyuru kasiin*

Translator: Pia kwa upande wa wakulima, wa angaliwe sana kuhusu mahindi. Sasa hakuna bei sasa wanaonelea ya kwamba kuweko na soko ya kuweza kuwasaidia sana kwa upande wa mahindi.

Jesalem Eleso: *Ompo wakulima, mchiini keros ngala ropyeen nyoman*

Translator: Watoto wasichana. Wasitahiriwe kama hawajamaliza masomo yao.

Com.: Na kumaliza ni standard gani?

Jesalem Eleso: *Ompo monuung chole tiipin kemuut otini kikuwany masomeengwaa.*

Translator: Ni university.

Jesalem Eleso: *Masomo nyopo paraak*

Translator: Pia yeye anataka kanisa lake liwe registered katika mafuta pole ile, vile ule mzee alisema.

Com: Sasa nikiangalia hapa naona kuna Noah chokorr. Lakini ni wa hiyo kanisa na memorandum ya kanisa tuko nayo. Kwa hivyo utatusamehe tupate mtu mwengine. Peter Yaralima, kutoka kalatorio, hayuko? Okey, kwa hivyo Noah Chokorr utatusamehe kwa sababu mzee wenu alizungumza na akatupatia memorandum, ambayo ni kubwa kabisa na tutaisoma yote. Emmuel Santos, Kabichibich youth, haya asante.

Translator: Anaitwa Emmanuel Santos.

Emmanuel Santo: *Kurenanuun Emannuel Santos*

Translator: Anataka sasa kuzungumza leo kwa sababu amepata uhuru.

Emmanuel Santo: *Omochan ongoloney aswaneete ompo wolo konyorwan kityaakat*

Translator: Kwa sababu tangu awali hapo hajaona uhuru pengine wengine wamepata lakini hapa hapana.

Emmanuel Santo: *Ompo wolo kungetaa kony, momiiiteni nyee huru nko yee*

Translator: Anataka watoto wote ambao wamemaliza form four, mpaka university waajiriwe wawe na mshahara. Wapate mshahara.

Emmanuel Santo: *Mchiini keto piich cho kikuwanya kopo angwan nko university keeto ropyeen.*

Translator: Kwa sababu wametumia pesa nyingi.

Emmanuel Santo: *Ompo wolo kikitumiyan ropyeen cho chang nyoman*

Translator: Katika sheria hii ya Kenya kile kilichochangia ukimwi kuenea zaidi ni ya mavazi yale wasichana wanavaa. Ni fupi sana, mpaka unaona watu wanaanza kukuwa na akili baya. Sasa anapendekeza hiyo, mambo kama hiyo, nguo ile fupi ipigwe marufuku kabisa.

Emmanuel Santo: *Mchiini yootuun, akiira katiba ompo Kenya loo mo mchiini nyee kulaak monuungo suroo cho tongoghoch*

Translator: Maana anataka muambiwe amna hiyo, sasa ile tamaa nyingi haitakuweco sasa ya kuenda ya ku-yape au ku-elope hata, itakwisha!

Emmanuel Santo: *Mchiini kukonyuut piich monuungo chole tiipin ato mokmiinyee puunoto nyopo tiipin.*

Translator: Haya.

Com.: Haya, tumpate Esther Mikaa yuko hapa? Hayuko Esther Mikaa? Richard Sinee?

Richard Sinee: Basi, asante sana Bwana Commissioner, mimi jina langu ni Richard Sinee kutoka Batei. Mimi ni mzee kutoka Batei location, katika constituency hii ya Sigor. Kwa sababu ya muda ambao pengine umetupa kisogo, nimetayarisha mapendekezo yangu kwa lugha ya kimombo. Na labda nitapitia haraka-haraka kwa kuyasoma. Now on political parties; The number of political parties should be limited to only two, like is the case of Britain and America. So as to bring to an end of formation of parties along the tribal lines. The two political parties should be financed by the state. The state should totally be de-linked from existing political parties. On structure and systems of the government, we should retain the unitary system of the government, in which all the affairs of the state are controlled by the Central Government, so that there are no imbalances in the control of natural resources and issue of domination by bigger tribes.

More powers should be vested with the elected representatives of the people at the district level who should also fully accountable to the people. On the electoral system and process, the constitution should provide for full participation of the electorate in the constituency demarcation, rather than influence from an individual politician like it happened way back from on the Lelan side. Because as you can see Lelan and Sigor are far apart, so it appears that people are not involved in demarcating this constituency. While deciding on additional constituencies, topography, geographical consideration should be of paramount importance just like that of population.

Many a times people talk of population in regardless of other issues like topography and geographical. Because even when we talk of a class, even if there are only two peoples it requires a teacher. Just like a class of a hundred pupils requires. Now, the election date is specified clearly in the constitution so that it is not used as a secret weapon by the incumbent President. Bribing

of voters should be outlawed in the constitution and deterrent punishment should be used.

On basic rights, and the rights of vulnerable groups, the constitution should provide for free and compulsory primary education for all Kenyan children. Two, the constitution should provide for a time frame, free secondary and university education for the marginalized communities like the Pokots, in line with government affirmative action, plan. And that is if they have to catch up with the rest of other Kenyans or else the Pokot or such tribes may remain cattle rustlers forever.

The constitution should provide for employment opportunities for the marginalized communities in like with affirmative action plan. While also sustaining the quota-system employment. The quota-system has really worked very well because way back, people use to come from other districts and get employed in this West-Pokot. So the quota-system should also be sustained. The constitution should provide for free medication, it has really been said. Now, the constitution should ensure provision of water in arid and semi-arid areas, it has already been said. The constitution should address the stone-age cattle rustling menace, in the North-Rift region. Especially through the formation of the commission of inquiry to get the root causes or causes and measure to combat it . And I would suggest that one such measure is education. If we can get educated, it will be long-term solution to this problem of cattle rustling.

And then to this end, the constitution should guarantee sustainable security. Land and property rights: The constitution should have the power, the government should have the power to compulsorily acquire private land for public use for which the owner should be compensated adequately. Two, the constitution should provide for a right to inheritance of land by unmarried women. Three the constitution should provide for free and wide distribution of the Kenya gazette notice to the Kenyan public all the time because it's a very important document, at the moment it is urgent to talk of Kenya gazette. People don't get it yet it carries very vital information.

Now, four, there should be legislation to limit the land owned by the individual person to say maximum of three thousand acres. Maximum, so that any extra land should be re-acquire by the state and re-allocated to benefit the landless and the squatters. People own large chunks of land at the moment, thousands. Now, the constitution should provide for compensation for land seized by the white settlers, unless is surrendered to the government. You may have heard maybe the day before people were talking about the Pokot having been driven from Trans-Nzoia, we feel that we should be compensated for that particular land, because we were pushed to the periphery.

Now, lastly there the Kenyans should not seek for land ownership beyond their respective provinces of birth. Say for that plot, because at the moment the constitution provides that you can settle anywhere in this country. But as it were, it appears there is a lot of movement, exodus of people from other pronvinces to the other provinces where people are still lagging behind.

Now, on cultural, ethnic, regional diversity and communal rights, I feel that mother tongue should be taught in primary schools

from one class to four, as a basic language. Secondly, the constitution should promote and recognize ethnic constitution where possible. We have very good constitutions, like our tribe. You remember the case of Nyalgunga and the rest, so we feel that our constitution should also be applied where it can work.

Management and use of natural resources: The government should have full control of all water catchments areas, rivers and swamps. The constitution should empower the local people through formation for committees, to take care of their respective district forests in conjunction with the forest personnel. Licencing of felling trees in the government forest and individual farms should be vested with the district, divisional and locational environment management committees, whose membership should comprise elected leaders and elders.

In the penal code on theft, we find it a bit absurd, where theft be it of stock, money motor vehicles are given different sentences.

We feel that it should be the same. At the moment, if one is found with the, you know, a problem of a stock theft, seven years, stealing millions of money, three years if it is not robbery with violence. We feel this should be the same, should be at par.

Now offenses related to marriage and domestic obligation, I feel and I can be corrected, the constitution is very very silent on penalty on adultery, it's not clear. Yet for Pokot constitution, at least there is penalty for that. So to contain the same, there should be a penalty for committing adultery. Offences against morality, in the penal code, I also feel that the law should provide for a penalty, preferably in form of compensation for impregnating a school girl, by a man, especially if such a girl will not be married. At the moment, it's silence, it's not clear.

And to wind-up on the constitution its-self, there is a lot of manipulation at the moment. I feel that any constitutional amendments. By Parliament, starting on the executive, on the legislature and judicature should first incorporate at least sixty-percent random public opinion, all to be carried out, throughout the eight provinces, by say the Attorney General and this is made to curtail the unpopular amendments likely to be sneaked in, such as; extending the term of the President, or life of Parliament, of awarding of M.P.s salaries and so on. And then on local government, I don't know if it has already been said, finally. Mayors and councilors should be elected directly by the people.

Com Lethome.: I am just asking, what is the penalty for adultery in Pokots' culture?

Richard Siree: It is valid from three to six heads of cattle, but it depends, if you go areas like Halale those sides, it's more there. So in this place, its valid from three to six, Thank you so much Bwana Commissioner.

Com Lethome. Sasa watu wa Lenal, tunawashukuru kabisa. Tunasema kila kitu ambacho ni kizuri kinafika mwisho wake. Mimi ningependa kutoka hapa mpaka saa sita ya usiku. Nikiwasikiza tu watu wa Lenal wakizungumza. Lakini hatuna budi

kuenda kwa sababu kesho tuko mahali pengine na leo tunapitia Sigor na mahali ingine kuchuchua watu. Na ile mashini, although imeundwa na mwanadamu, mvua ikinyesha haiwezi kuruka hapa itatuletea taabu. Pilot ametuambia saa kumi lazima tuondoke, lakini kila mtu ambaye alikuwa mumejiandikisha anataka kuzungumza, amezungumza. Kitu moja nataka kuwaambia watu wa Lenal, tangu tulipoanza kazi Rift-Valley, North Rift, hakuna watu wengi mumejiandikisha kama nyinyi. Mumejiandikisha watu mia tatu na sabini, three hundred and seventy that is a record.

Na wale wamezungumza, ni watu sitini. Wale wametoa maoni yao ni maoni ya hali ya juu sana. It's quality views that we have heard today. Tumepata maoni ya hali ya juu sana hata tumekuwa kama tuko skuli tunafundishwa mambo mapya ambayo hatujaskia. Kwa hivyo tunawashukuru sana na ningependa kuwajulisha huu si mwisho wa kutoa maoni. Kuanzia sasa mpaka kufika mwisho wa mwezi wa saba. Ikiwa una maoni yoyote ambayo ungependa kufikisha kwetu. William yuko hapa yeye ni katika 3 C members. Wao ni wawakilishi wetu hapa. Mfikishe kwao maoni kwa maandishi, itatufikia kwa sababu yeye atafikisha kwa district co-ordinator na district coordinator atatufikishia huko Nairobi. Hebu waambie hiyo kwa ufupi sana kwa lugha ya nyumbani.

Halafu pia ningependa kuwajulisha kuna watu wengine wana wasiwasi. Wanasema tunayo haya maoni halafu yatapotea. Tunawajulisha kuwa sheria imetulazimisha sisi baada ya kuchukua hii maoni yenu yote, tunaandika report, halafu hiyo report yatachapishwa kwenya vitabu kama kile chekundu ambacho naona watu wengine wako nayo. Yatarudi kwenu, yatazunguka kwa muda wa mwezi mmoja au miezi miwili, mutaangalia maoni yenu yamefika huko ama hayajafika. Ndio sababu unaona tunarekodi, unaona tangu tulipokuja hapa, tunaandika kwa sababu hatutaki kupoteza maoni ya mtu yeyote. Kwa hivyo, tunawahakikishia maoni yenu mtaona wenyewe vile yamefika huko.

Asante, kwa hivyo sasa tunawashukuru nyote kwa vile mumekuwa kwa wingi na maoni yule ambayo mumetowa. Na mjue wale wote wamezungumza wametengeneza historia. Hata baada ya miaka mia moja, watoto watakuwa wakisoma wanaona hapa Mary alizungumza, kuna mzee alizungumza. Hiyo ni historia.

Tunashukuru wale wote ambao wamepanga mkutano hapa leo, tunawashukuru na viongozi ambao wamewacha kazi zao, wakaja hapa wale members wa three C's wale waliosomesha watu civic education, tunajua muna matatizo ya pesa kwa sababu budget ya civic education ilikuwa ni ndogo sana.

Hiyo complaint tumepata kila mahali tumeenda na commission inajaribu kuangalia vile inaweza kufanya, idara yetu inaangalia huko. Kwa hivyo, tunawashukuru nyote. Mungu awabariki. Ningependa sasa kumwachia William, naona kuna mzee ana mkono juu, mzee hebu sema kuna shida gani?

Mzee: Asante sana Bwana Commissioner, swali langu ni kwamba, kuna tatizo kubwa ambalo pia hatujatosheka ambao tungetaka utueleze kama Commissioner ya kwamba, maoni haya tunayotoa, labda tu itakuwa ni ya kuzungumza hapa halafu

pengine yasitokee katika katiba ambayo itakaandikwa.

Com Lethome: Sasa mzee, wacha nisimame sasa. Kwa sababu mini sio mama wa Kipokot. Ndio wanaambiwa wakae chini, mimi nitasimama. Nimesema hapa, taratibu ya sheria imeweka taratibu mbili za kuhakikishia Wakenya kuwa yale maoni wanayotoa hayatapotea. Taratibu ya kwanza; ni kuwa baada ya sisi kukusanya hii reporti yote, na ndio unaona kuna sign nyingi hizo. Tunapeleka kwa commission, kuna watu wataandika hiyo yote iwe ni report. Hiyo report itarudishwa kwenyu wananchi, mtakaa nayo muangalie kwa muda wa mwezi moja ama miwili, munaangalia tu! Maoni yenu yamefika ama hayajafika, hiyo taratibu ya kwanza, hebu waambie hiyo!.

Ya pili, ya pili kuna kitu inaitwa National Constitutional conference. Kuna mzee mmoja kutoka Cherenga'ny alizungumzia hiyo. Tumeambiwa kuwa baada ya hiyo report kuzunguka kwenyu na kurudi Nairobi tena, baada ya nyinyi kuhakisha maoni yetu yameandikwa, kuna mkutano ambao inaitwa National conference, utafanyika Nairobi. Mkutano wa miezi mbili, nafikiria katika historia ya Kenya hakujatokea mkutano kama hiyo, mkutano ya miezi mbili. Na katika historia ya Kenya, hakujatokea mkutano kama huo, mkutano ya miezi miwili. Na katika huo mkutano, M.Ps wote watakuweco, kwa hivyo M.P. Wenu atakuwa katika huo mkutano. Halafu katika kila district, kutoka district yenu kutatoka watu watatu, mtachangua watu watatu, watakuja huko. Halafu mtachangua kutoka political parties mtu mmoja mmoja. Kina mama, organizations za kina mama, mtu mmoja mmoja. Religious organization, watu wa dini, mtu mmoja mmoja, youth, mtu mmoja mmoja. Kama muko na organization zengine kama za wakulima, professional bodies kama walimu, kama vile kuna KNUT, na zingine watakaa huko. Watu karibu mia sita watakaa miezi miwili, kujadiliana hayo maoni kabla hayajaandikwa kwa katiba mpya.

Hiyo ndiyo taratibu imewekwa na sheria, kuhakikisha hakuna kitu inapotea. Tunajuwa Kenya, Commission nyingi zinafanya kazi inapotea, watu hawajui imefika wapi. Hii inakuhakikishia utaona matunda yake ukiwa hai.

William: Basi waheshimiwa Macommissioners napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru nyinyi sana. Kwa kuweza kufika hapa leo na kupokea maoni yetu. Pelekeni maoni yetu na muweke vile mumesema ili sisi watu wa Lelan tufurahi. Basi, kwa niaba ya hawa watu kuruhusu sisi kutumia hall yao ya hata wale watoto wadogo.

Kuna hapa ni nursery school, mahali walikuwa wakosomea, tuliweza kukatisha kidogo. Kwa hivyo tunashukuru sana father ya hapa kwa kuturuhusu na kwa kukubali. Na vile vile, ningependa kuwashukuru sana wananchi wa hapa, wa kusikia mwito ambao kwa muda mfupi, tuliweza kumobilize hawa waje, ili watoe maoni. Na mimi ninashukuru sana, wakati mwingine jambo fulani likitokea ambalo tunahitajika tuje kwa wingi nanma hii. Kwa hivyo vilevile ninaweza kushukuru, C.C.C. wa Sigor constituency vile mimi ni mwenyekiti wao, ningependa kushukuru hao sana kwa cooperation ambayo walitoa kwa kushughulika.

Sisi, tuligawa kazi, sisi watu watatu upande huu na wengine Sigor, kwa sababu ya umbali. Kwa hivyo wale walifanya huko, nafikiri wamefanya bidii na sisis upande huu vile vile ninawashukuru hawa kabisa, hawa ni walimu, wana kazi nyingi mara nyingi

wana organise huko na wanarudi shule. Mfano Mary anafundisha shule ya secondary school huko Tartar, na alifanya kazi nyingi sana, aliweza kujaribu kabisa, kwa hivyo waheshimiwa commissioners, bila kupoteza wakati kwa maombi yetu sasa tutatumia maombi ya mzee wa kienyeji, ili muende na baraka ya Pokot. Mrudi tena mkumbuke nchi ya Pokot, wanaishi namna gani, utamaduni yao na kila kitu, kwa hivyo, kwa hayo machache, ninakaribishe huyu mzee, asante.

Elder: Maombi in Kipokot.

Soro, soro, soro, soro, aitech kooree, soro soro